VISION 2050

SEPTEMBA 15, 2026 /islamicftz

Rabi ul-Thani 4 1448

# IMAAN

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

ISSN 5618 - NO. 601



## Mwinyi, Othman: Sasa tujenge Z'bar mpya

# Watanzania wamkumbatia Rais Samia katika majonzi

**Katika majonzi ya kumpoteza mumewe, Rais Samia amezungukwa na wimbi la mshikamano, huku Watanzania wa dini, kada na makundi mbalimbali wakifika Kizimkazi kumpa faraja, dua na pole.**



Mwenyekiti wa The Islamic Foundation (TIF), Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri (CIFCA), Aref Nahdi, na viongozi wengine wakimfariji Rais Dk. Samia Suluhu Hassan nyumbani kwake, Kizimkazi baada ya kufiwa na mumewe.

Kenya yatakiwa kubadili kanuni kukuza benki za Kiislamu »

Samia Scholarship yawafungulia vijana 150 kusoma Algeria »

# Mwinyi: Kheri haipimwi kwa fedha pekee

**Awataka Waislamu kutambua kuwa kila mmoja ana cha kujitolea, kwa mali, muda, elimu, nguvu na dua, ambavyo ni msingi wa kujenga jamii yenye kheri, umoja na amani**

**... awataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya El Niño**



TCRA yaongeza nguvu kudhibiti utapeli wa simu Moro

فتاوى SHEIKH Shaaban Mussa

# Nchi 8 za Kiislamu zataka hatua kali dhidi ya Israel

NA ABUU HAYTHAM HASSAN, MORO

# The Islamic Foundation yaja na mkakati kutekeleza Dira ya Taifa 2050




MENEJIMENTI ya The Islamic Foundation yenye makao makuu yake mjini Morogoro imefanya kikao maalumu kwa ajili ya kuweka mikakati ya utekelezaji wa shughuli zinazogusa moja kwa moja maendeleo ya wananchi kwa namna chanya.

Taasisi hiyo imeandaa mkakati huo ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika kuunga mkono Serikali katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Dira hiyo ilipitishwa na Baraza la Mawaziri mwaka 2025 kabla ya kuwasilishwa Bungeni Juni 26 mwaka huo, na baadaye kuzinduliwa rasmi na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan Julai 17, 2025, jijini Dodoma. Utekelezaji wake ulianza rasmi Julai 1, 2026.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kuijenga Tanzania kuwa Taifa jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea, likiwa na uchumi imara na wananchi wenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo.

Pia, Dira hiyo inalenga kuiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi yenye kipato cha kati cha juu na kujenga uchumi wenye thamani ya dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

Akizungumza na Gazeti Imaan baada ya kikao hicho, Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amesema taasisi hiyo imeona umuhimu wa kupanga shughuli zake kwa namna itakayowezesha mchango wake kuonekana moja kwa moja katika maisha ya wananchi na katika kufikiwa kwa malengo ya Taifa.

Amesema The Islamic Foundation itaendelea kuelekeza nguvu katika programu zinazolenga kuwajengea wananchi uwezo wa kujitegemea, kuwawezesha vijana na makundi yenye uhitaji, pamoja na kuchangia katika maeneo ya elimu, maarifa, ujuzi na ustawi wa jamii.

Nahdi amesema utekelezaji wa Dira 2050 unahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali na kwamba taasisi za kijamii zina nafasi ya kutumia uwezo, uzoefu na rasilimali zilizonazo kusaidia kuongeza kasi ya maendeleo.

Amesema pamoja na maendeleo ya kiuchumi na kijamii, amani na mshikamano ni miongoni mwa misingi muhimu inayoweza kuwezesha Taifa kufikia malengo yake.

Kwa mujibu wake, wananchi wanahitaji mazingira ya amani, umoja na utulivu ili waweze kufanya kazi, kuendesha shughuli za kiuchumi na kutumia fursa zinazopatikana katika maeneo yao.

The Islamic Foundation imeeleza kuwa itaendelea kuoanisha shughuli zake za maendeleo ya jamii na vipaumbele vya Dira 2050, ikiwa ni sehemu ya wajibu wake wa kuchangia katika kujenga jamii yenye elimu, ujuzi, maadili na uwezo wa kujitegemea.

Hatua hiyo inaendana na msisitizo wa Serikali kwamba utekelezaji wa Dira 2050 unahitaji ushiriki wa taasisi na wadau mbalimbali ili malengo yake ya muda mrefu yaweze kufikiwa.

# Watanzania wamkumbatia Rais Samia katika majonzi

WATANZANIA wa kada, dini na makundi mbalimbali wameonyesha mshikamano na upendo mkubwa kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakimzunguka kwa faraja, dua na salamu za pole kufuatia kifo cha aliyekuwa mumewe, Mzee Hafidh Ameir Hassan.

Mzee Hafidh alifariki Septemba 7, 2026 mjini Zanzibar, na tangu wakati huo nyumbani kwa familia ya Rais, Kizimkazi, Kusini Unguja, kumekuwa na msururu wa waombolezaji kutoka maeneo mbalimbali nchini na nje ya Tanzania.

Mwitikio huo umekuwa ishara kubwa ya namna Watanzania wanavyompenda Rais wao na hivyo kuguswa na msiba huo wa mumewe, ikithibitika kwa namna viongozi, taasisi na wananchi wa makundi mbalimbali wakifika au kutuma salamu za pole na kumuombea yeye na familia yake.

Katika ujumbe wa shukrani uliotolewa na Ikulu, Rais Samia alisema yeye na familia yake wameguswa na faraja, dua na maombi yaliyotolewa na Watanzania pamoja na marafiki wa Tanzania kutoka sehemu mbalimbali duniani.

"Katika kipindi hiki cha majonzi, faraja yenu imekuwa sehemu ya nguvu yetu," familia ilieleza katika ujumbe wake.

Miongoni mwa waliokwenda Kizimkazi ni viongozi wakuu wa Serikali, wakiwamo Makamu wa Rais, Deogratius Ndejembi; Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi; Waziri Mkuu, Dk.t Mwigulu Nchemba; na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Moses Kusiluka na karibu baraza zima la mawaziri,

Mshikamano huo ulivuka pia mipaka ya Tanzania, viongozi kutoka mataifa mbalimbali, wanadiplomasia na maofisa wa taasisi za kimataifa wakifika Kizimkazi kutoa pole miongoni mwao Rais wa DR Congo, Felix Tshisekedi; Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye; pamoja na wawakilishi kutoka Oman, China, Türkiye na taasisi za kimataifa.

Ukiacha wageni hao, karibu mabalozi wengi wanaowakilisha nchi zao hapa Tanzania pia walienda Zanzibar katika nyakati tofauti kumpa pole Rais Samia,

Viongozi wa dini nao walikuwa sehemu muhimu ya msururu wa waombolezaji. Karibu viongozi wa makanisa yote makubwa walienda Zanzibar kumuunga mkono Rais katika wakati huu wa huzuni lakini miongoni mwao walikuwepo Boniface Mwamposa na Tony Kapola.

Mwitikio mkubwa zaidi umeonekana kutoka kwa viongozi na taasisi za Kiislamu, ambao nao kwa wingi waliungana na Watanzania wengine kumpa Rais Samia faraja katika kipindi hicho.

Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, naye alifika Kizimkazi kutoa pole. Nahdi pia ni Mwenyekiti wa CIFCA ni Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri nchini Tanzania, taasisi inayojihusisha na maendeleo na usimamizi wa masuala ya fedha za Kiislamu, pamoja na kuwa Mweka Hazina wa Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA).

Taasisi nyingine za Kiislamu zilizojitokeza ni Jumuiya ya Wataalamu wa Kiislamu (TAMPRO) inayowaunganisha wanataaluma Waislamu nchini; Umoja wa Maimamu Tanzania (UMATA); pamoja na Umoja wa Shule za Msingi za Kiislamu Tanzania (TIPSO).

Viongozi wengine waliofika ni Sheikh Ponda Issa Ponda wa Shura ya Maimamu Tanzania. Katika taratibu za mazishi, Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, ndiye aliyeongoza Sala ya Jeneza ya marehemu.

Ushiriki mpana wa viongozi hao umeonyesha namna taasisi tofauti za Kiislamu zilivyoungana katika dua na faraja kwa familia ya Rais, sambamba na viongozi wa madhehebu mengine ya dini waliojitokeza.

Sekta binafsi, michezo na burudani nazo hazikubaki nyuma. Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank, Dk. Abdulmajid Nsekela; Mkurugenzi Mtendaji wa Amsons Group, Edha Nahdi; viongozi wa michezo na kijamii walijumuika na waombolezaji.

Kwa jumla, msiba wa Mzee Hafidh umeonyesha sura ya jamii ya Kitanzania ambayo katika nyakati za huzuni huweka mbele utu, faraja na mshikamano.

Kwa Rais Samia, wingi wa waliofika, waliotuma ujumbe na waliomuombea umebeba ujumbe mmoja mkubwa: katika wakati wake wa majonzi, Watanzania wamesimama naye na familia yake.





SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Je mwanamke anaweza kwenda kazini wakati wa eda?

**Swali: Naomba kuelimshwa kuhusu mwanamke aliyefiwa na mumewe anatakiwa kukaa edani kwa muda gani? Je, akiwa ni mtumishi wa umma, daktari, mwalimu, meneja au mwenye kazi nyingine maalum inayohitaji kuhudumia watu, anaruhusiwa kutoka nyumbani kwenda kazini wakati wa eda yake? Na je, ikiwa kazi yake ni ya muhimu kwa jamii, hukumu inabadilika?**

**Jibu:** Mwanamke aliyefiwa na mumewe anatakiwa kukaa katika eda yake kwa muda uliowekwa na Sharia. Ikiwa si mjamzito, eda yake ni miezi minne na siku kumi, kama Allah Mtukufu alivyosema: "Na wale miongoni mwenu wanaofariki na wakaacha wake, wake hao wajizuie kwa muda wa miezi minne na siku kumi." [Qur'an, 2: 234].

Ikiwa mwanamke huyo ni mjamzito, eda yake huisha pale atakapojifungua. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Aliyetukuka: "Na wanawake wenye mimba, muda wao wa eda ni mpaka wajifungue." [Qur'an, 65: 4].

Hata hivyo, kukaa edani hakumaanishi kwamba mwanamke haruhusiwi kabisa kutoka nyumbani kwa hali yoyote. Msingi ni kwamba akae katika nyumba aliyokuwa akiishi wakati mumewe alipofariki, lakini anaweza kutoka kwa haja inayotambulika kisharia, kisha arejee nyumbani kwake.

Kwa hiyo, ikiwa mwanamke ni mtumishi wa umma, mwalimu, daktari, meneja, mfanyakazi au mwenye kazi nyingine halali, si lazima aache kazi yake kwa kipindi chote cha eda ikiwa kuna haja ya kuendelea na kazi hiyo na hawezi kuipumzisha bila kupata madhara makubwa kwake au kwa wengine.

Aliyekuwa Mufti wa Saudi Arabia Sheikh ʿAbdul-ʿAziz ibn Baz, (Allah amrehemu), alieleza kwamba mwanamke aliye katika eda ya kufiwa anaweza kwenda kwenye kazi yake inapokuwa ni haja yake; akatoa mfano wa mwajiriwa na mwalimu anayekwenda kazini kisha anarudi nyumbani.

Hivyo, kuwa katika eda hakumaanishi kupoteza ajira wala kusimamisha kila shughuli ya maisha, bali kunamaanisha kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sharia katika kipindi hicho.

## Masharti matano ya kuchunga

Lakini ruhusa ya kutoka kwenda kazini si ruhusa ya kutoka bila mipaka. Mwanamke anatakiwa achunge masharti au mipaka matano ikiwemo kwanza, atoke kwa haja halisi, kama kazi ambayo anahitaji kuifanya na hakuna njia nyimgine ya kuikwepa au kupata mtu wa kumwakilisha.

Sharti la pili, atoke kwa muda unaohitajika, na akimaliza kazi arudi nyumbani; na sharti la tatu, alale katika nyumba yake ya eda, isipokuwa kama kuna dharura au haja nyingine inayotambuliwa kisharia.

Sharti la nne, ni lazima aende kazini akiwa katika hali ya 'ihdad', yaani kuacha mambo ya kujipamba kwa ajili ya mume aliyefariki, kama kutumia manukato, kuvaa mapambo na mavazi yanayokusudiwa kujipamba na tano na mwisho, aendelee kuzingatia heshima, sitara na mipaka ya Sharia katika mazingira ya kazi.

Na ikiwa mwanamke huyo ana jukumu maalumu la kuhudumia jamii, kama daktari, mwalimu, meneja wa taasisi, mtumishi wa umma au mwenye nafasi ambayo kutokuwepo kwake kunaweza kusababisha madhara kwa watu, haja hiyo inaweza kuzingatiwa zaidi. Lakini haimaanishi kwamba kwa sababu tu ni mtumishi wa umma basi masharti ya eda yanaondoka.

Kwa ufupi: Eda haiondolewi kwa sababu ya kazi. Lakini kazi halali na haja inayotambulika inaweza kuwa sababu ya kuruhusiwa kutoka wakati wa eda.

Kwa hiyo, mwanamke aliyefiwa na mumewe anatakiwa kuendelea na eda yake kikamilifu, huku akitoka kwa mahitaji muhimu, yakiwemo kazi, inapokuwa kuna haja ya kufanya hivyo, na kurudi nyumbani baada ya kumaliza haja yake.

Jambo la msingi ni kutofautisha kati ya "kutoka kwa haja" na "kuacha kukaa edani." La kwanza linaweza kuruhusiwa kwa masharti; la pili si sahihi. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

NA MWANDISHI WETU

# TCRA yaongeza nguvu kudhibiti utapeli wa simu Morogoro



## Kilombero kitovu cha uhalifu kwa njia ya simu

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeongeza kasi katika mapambano dhidi ya utapeli wa simu na uhalifu mtandaoni, ikiwa imeendesha kampeni ya siku tatu ya uhamasishaji katika Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro.

Kampeni hiyo, inayomalizika leo, imefanyika kwa ushirikiano na wadau mbalimbali, ikilenga kuongeza uelewa wa wananchi na watumishi wa Serikali kuhusu namna ya kujikinga na uhalifu wa kimtandao, huku ikija wakati idadi ya matukio hayo ikiendelea kuwa kubwa katika baadhi ya maeneo licha ya kupungua kitaifa.

Akizungumza jana katika semina iliyowakutanisha watumishi wa Serikali mjini Ifakara, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Peter Mwasalyanda, alisema mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mawasiliano yanapaswa kulindwa dhidi ya wahalifu wanaotumia teknolojia za kidijitali kutekeleza uhalifu.

Alisema idadi ya matukio ya utapeli na ulaghai yanayofanywa kupitia simu za mkononi ilipungua kwa asilimia 25.29, kutoka matukio 9,816 katika robo mwaka iliyoishia Machi 2026 hadi 7,334 katika robo mwaka iliyoishia Juni mwaka huu.

"Pamoja na kupungua huko, hali bado inatia wasiwasi katika baadhi ya maeneo, hususan mikoa ya Morogoro na Rukwa, ambako idadi ya matukio yaliyoripotiwa bado ni kubwa," alisema.

Kwa mujibu wa Mwasalyanda, kati ya matukio 7,334 yaliyoripotiwa nchini katika kipindi hicho, Morogoro ilikuwa na matukio 2,079, sawa na asilimia 28.4, huku Rukwa ikiwa na matukio 2,495, sawa na asilimia 34.



Katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero pekee ilirekodi matukio 1,778, ambayo ni sawa na asilimia 86 ya matukio yote yaliyoripotiwa mkoani humo.

Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa kwa ujumla matukio hayo yamepungua kwa asilimia 69 tangu Septemba 2023, ambapo yalifikia 23,328, hadi kufikia 7,334 Juni 2026.

Mwasalyanda alieleza kuwa uhalifu wa kimtandao unajumuisha utapeli mtandaoni, wizi au matumizi yasiyoidhinishwa ya taarifa, udukuzi, ulaghai wa kielektroniki, usambazaji wa programu hasidi pamoja na matumizi mabaya ya akaunti na mifumo ya kidijitali.

Alisema vitendo hivyo vinaweza kuhatarisha usalama wa watu binafsi, taasisi na hata usalama wa taifa. Alisema kampeni hiyo inalenga kuwajengea uelewa watumishi wa Serikali na wananchi kuhusu uhalifu wa kimtandao na usalama wa huduma za mawasiliano, pamoja na kuwaelimisha kuhusu hatua za kuchukua ili kujilinda dhidi ya utapeli wa mtandaoni.

Mwasalyanda aliwataka Watanzania kuwa waangalifu wanapotumia majukwaa ya kidijitali na kujenga utamaduni wa kuzingatia usalama wa mtandao.

"Hatupaswi kuishia kuwa na mifumo salama pekee; tunahitaji pia watu wenye uelewa wa kutosha wa namna ya kutumia mifumo hiyo kwa usalama," alisema.

NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi, Othman: Sasa tujenge Zanzibar mpya

Hatua mpya ya utekelezaji wa makubaliano ya kisiasa ya maridhiano Zanzibar imeanza baada ya kuundwa kwa kamati ya watu 10 itakayoratibu utekelezaji wa tamko la pamoja la CCM na ACT-Wazalendo.

Kamati hiyo ilizinduliwa jana, Jumatatu, Septemba 14, 2026, Ikulu Zanzibar na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Mwinyi, kufuatia tamko la pamoja lililosainiwa na vyama hivyo Julai 9, mwaka huu.

Tamko hilo limeelezwa kuwa msingi wa kuimarisha amani, umoja na ushirikiano wa kisiasa Zanzibar, huku kamati hiyo ikipewa jukumu la kuratibu utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa na vyama hivyo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo, Dk Mwinyi alisema kuundwa kwake ni ishara ya ukomavu wa kisiasa na kuwataka wajumbe kutoka CCM na ACT-Wazalendo kuweka maslahi ya Zanzibar mbele kuliko maslahi ya vyama vyao.

"Ninawasihi wajumbe walioteuliwa kutoka CCM na ACT-Wazalendo kutumia uzoefu, ujuzi na uwezo wao kuhakikisha kazi hii inakamilika kwa ufanisi," alisema Dk Mwinyi.

Alisema wananchi wanatarajia siasa zitumike kujenga amani na maendeleo badala ya kuwa chanzo cha migawanyiko.

"Wananchi wanataka kuona amani na maendeleo katika maisha yao ya kila siku," alisema. Dk Mwinyi pia aliwatambua viongozi wa zamani wa Zanzibar, Amani Abeid Karume na Ali Mohamed Shein, kwa mchango wao katika mchakato wa maridhiano ya kisiasa visiwani humo.

Alisema kamati hiyo imepewa muda wa miezi mitatu kukamilisha kazi yake, ingawa muda huo unaweza kuongezwa iwapo kutakuwa na sababu za msingi.

Othman ataka simulizi mpya

Kwa upande wake, kiongozi wa ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, aliitaka kamati hiyo kusaidia kujenga kile alichokiita "simulizi mpya" ya Zanzibar, akisisitiza kuwa maridhiano ya kisiasa ni muhimu kwa ustawi wa uchumi na kuvutia uwekezaji.

Othman, ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa zamani wa Zanzibar, alisema utulivu wa kisiasa ni msingi muhimu kwa uchumi wa Zanzibar unaotegemea kwa kiasi kikubwa sekta ya huduma na uwekezaji.

Alisema wawekezaji huwa waangalifu wanapowekeza fedha zao katika maeneo yasiyo na utulivu, hivyo Zanzibar inapaswa kujenga mazingira salama na ya kuaminika kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

"Mtu mwenye fedha ni mwangalifu sana; hawezi kupeleka fedha zake mahali ambapo hakuna utulivu," alisema Othman.

Aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kuweka pembeni maslahi ya vyama na kuelekeza nguvu zao katika maslahi mapana ya taifa, akisisitiza umuhimu wa Zanzibar kujifunza kutokana na yaliyopita na kuepuka kurudia makosa ya zamani.

Kamati hiyo inaongozwa kwa pamoja na Omar Ali Shehe wa ACT-Wazalendo na Abdi Mahmoud Abdi wa CCM.

Akizungumza kwa niaba ya kamati, Shehe aliwahakikishia Wazanzibari kuwa wajumbe wataendesha kazi hiyo kwa uadilifu, huku akijibu hoja kuhusu uteuzi wa makada wa vyama katika kamati hiyo.



UKHTI FATIMA SS




# Samia Scholarship yawafungulia vijana 150 kusoma nchini Algeria

Tanzania imepata nafasi 150 za ufadhili wa masomo nchini Algeria zitakazotolewa kwa wanafunzi waliofanya vizuri Kidato cha Sita kupitia mpango wa Samia Scholarship.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali ya Algeria itagharamia ada za masomo ya wanafunzi hao, wakati Tanzaniaitabeba gharama za maisha na fedha za kujikimu.

Profesa alisema fursa hiyo inawapa nafasi wanafunzi wenye uwezo mkubwa kitaaluma kusoma katika mazingira ya kimataifa, hususan katika fani za sayansi.

Alisema majina ya wanafunzi hao 150 yatachapishwa kwenye tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na maelekezo kuhusu uwasilishaji wa nyaraka na kukamilisha taratibu za safari, ikiwemo upatikanaji wa hati za kusafiria.

Aliwataka wanafunzi hao kujiandaa kukabiliana na mazingira mapya ya masomo, ikiwamo kujifunza lugha ya Kifaransa, inayotumika kwa kiasi kikubwa katika mfumo wa elimu nchini Algeria.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Algeria, Mobhare Matinyi aliishukuru Serikali ya Algeria kwa kuongeza nafasi za wanafunzi wa Tanzania mwaka huu kutoka 45 mwaka jana, akisema kuna uwezekano wa nafasi hizo kuongezeka zaidi mwakani..

Baadhi ya programu muhimu watakazojiunga nazo vijana hao ni kilimo, afya, sayansi ya data na teknolojia, husused Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Habari hii njema inakuja wakati kati ya wanafunzi 1,000 waliotangazwa kupata ufadhili kupitia Samia Scholarship, 10 mwezi uliopita walitangazwa kupata nafasi ya kwenda kusoma Moscow, Urusi.

NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi atoa tahadhari ya El Niño



## ■ Atoa tahadhari kali kwa wananchi kujikinga na athari za El Niño na mvua kubwa, huku akiagiza Serikali kuimarisha maandalizi, usafishaji wa mifereji na utoaji wa taarifa sahihi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wananchi kuchukua tahadhari mapema dhidi ya athari zinazoweza kusababishwa na hali ya El Niño na mvua kubwa zinazotarajiwa kunyesha, huku akizitaka taasisi za Serikali kuimarisha utoaji wa elimu na taarifa sahihi kwa umma.

Rais Dkt. Mwinyi alitoa wito, Septemba 11, 2026, muda mfupi baada ya Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Masjid Swafaa, Gongoni, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema wananchi wanapaswa kufuatilia kwa karibu taarifa rasmi za hali ya hewa pamoja na maelekezo yanayotolewa na Serikali na mamlaka husika, badala ya kupuuza tahadhari zinazotolewa kuhusu maeneo yanayoweza kuathiriwa na mvua kubwa.

Aliwataka wananchi kuepuka maeneo hatarishi, yakiwemo mabondeni, mikondo ya maji na njia za maji, huku akisisitiza umuhimu wa kuhama mapema kutoka maeneo yaliyo katika hatari pale mamlaka zitakapotoa maelekezo ya kufanya hivyo.

"Wananchi wanapaswa kufuatilia taarifa na maelekezo rasmi kutoka Serikali na mamlaka husika, na kuchukua tahadhari zinazohitajika," alisema.

Katika hatua nyingine, Rais Mwinyi amezitaka Manispaa zote za Unguja na Pemba kuhakikisha mifereji ya maji na njia zinazopitisha maji zinasafishwa mapema ili kupunguza uwezekano wa kutokea kwa mafuriko na madhara yake.

Alisema maandalizi hayo yanapaswa kufanyika kabla ya mvua kubwa kuanza, akisisitiza kuwa usafi wa mifereji na njia za maji ni sehemu muhimu ya hatua za kuzuia na kupunguza athari za mafuriko.

Rais Mwinyi alisema Serikali imejiandaa kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na hali hiyo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uwezo wa uokozi, kutoa msaada kwa wananchi watakaokumbwa na madhara na kuhakikisha huduma muhimu zinaendelea kupatikana.

Alisema Serikali pia imeweka mkazo katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula na dawa unalindwa, hususan katika maeneo ambayo yanaweza kukumbwa na mafuriko au changamoto za usafiri na mawasiliano.

Aidha, alisisitiza kuwa taasisi zote zinazohusika na uokozi, huduma za kijamii na kukabiliana na majanga zinapaswa kuwa katika hali ya utayari wakati wote ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma na msaada kwa wakati pale changamoto zitakapotokea.

Wito huo unakuja wakati mamlaka zikitoa tahadhari kuhusu uwezekano wa mvua kubwa, hali inayoweza kuongeza hatari ya mafuriko, uharibifu wa miundombinu na athari nyingine kwa shughuli za kijamii na kiuchumi.

Rais Mwinyi aliwataka wananchi kutoupuuza ujumbe wa tahadhari, akisisitiza kuwa maandalizi ya mapema, ufuatiliaji wa taarifa sahihi na ushirikiano kati ya wananchi na Serikali ni muhimu katika kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

# MIMBARI ZETU

IMEANDALIWA
Na Barnabas Mkwayu
0766 364 354

## KUTOKA

Msikiti wa Mtume
**(Madina)**

Msikiti Maamour
**(Upanga, Dar es Salaam)**

Msikiti Imaam Bukhary
**(Morogoro)**

Masjid Al-Haram
**(Makka)**



## MASJID AN-NABAWI



# Imam Madina aonya dhidi ya udanganyifu katika biashara

IMAMU na Khatibu wa Msikiti wa Mtume, Madina, Sheikh Dkt. Hussein Aal Al-Sheikh, amewaonya Waislamu dhidi ya udanganyifu katika biashara, akisema uaminifu, ukweli na kutimiza ahadi ni misingi muhimu ya Uislamu.

Akitoa khutba ya Ijumaa Septemba 11 katika Masjid an-Nabawi, Sheikh Hussein alisema Shariah imeharamisha udanganyifu wa aina zote kutokana na madhara yake kwa watu katika chakula, vinywaji, mavazi, magari na bidhaa nyingine.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Saudi Arabia (SPA), Sheikh Hussein alisema udanganyifu si kosa la biashara pekee, bali unaweza kuwa chanzo cha madhara makubwa kiafya, hasa pale bidhaa bandia au zenye kasoro zinapouzwa bila kueleza ukweli.

Alisema baadhi ya aina za udanganyifu zinaweza kusababisha magonjwa makubwa na madhara ya muda mrefu kwa watumiaji.

Sheikh Hussein alikumbusha Hadith ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) inayosema: "Mwenye kutudanganya si katika sisi."

Pia alisema kuchukua fedha za watu kwa kuuza bidhaa zenye kasoro zilizofichwa ni kula mali za watu kwa batili na kuwadhulumu.

Kwa mujibu wa khutba hiyo, wajibu wa uaminifu hauishii kwa wafanyabiashara pekee. Kila mtu mwenye dhamana au jukumu linalogusa maslahi ya wengine anatakiwa kulitenda kwa uaminifu, ikiwamo viongozi, wasimamizi na watoa huduma.

Sheikh Hussein alisisitiza kuwa Muislamu anayemuuzia mwenzake bidhaa yenye kasoro anatakiwa kueleza kasoro hiyo wazi kabla ya mauzo kukamilika.

Katika sehemu ya mwisho ya khutba, aliunganisha ukweli na baraka katika riziki.

Alinukuu Hadith inayosema wauzaji wawili wakisema kweli na kuweka wazi hali ya bidhaa, biashara yao hubarikiwa; lakini wakidanganya na kuficha ukweli, baraka ya biashara yao huondolewa.

Sheikh Hussein aliwataka Waislamu kuwa waaminifu katika maneno, vitendo na miamala yao yote, akisisitiza kuwa biashara yenye baraka hujengwa juu ya ukweli, uwazi na uaminifu.

## MASJID MAAMOUR, UPANGA



# Imam aonya: Haitoshi kujua kuisoma, tuiishi Qur'an

WAISLAMU wametakiwa kutotosheka tu na kusoma au kuhifadhi Qur'an, bali wajifunze maana yake na kuyatekeleza maamrisho na makatazo yaliyomo ndani yake.

Akitoa Khutba ya Ijumaa ya Septemba 11, 2026, Imam Mkuu wa Msikiti Maamour uliopo Upanga jijini Dar es Salaam, Sheikh Issa Othman alisema kuwa Maswahaba (Allah awaridhie) walikuwa wakijifunza Qur'an kwa hatua, wakihakikisha wameelewa na kutekeleza walichojifunza kabla ya kuendelea na aya nyingine.

Alinukuu maelezo ya Maswahaba waliokuwa wakisema kuwa walijifunza imani kwanza, kisha Qur'an, jambo lililowasaidia kuongeza imani yao.

Kwa mujibu wa khutba hiyo, baadhi ya Maswahaba walikuwa wakijifunza aya 10 kutoka kwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) na hawakuendelea na aya nyingine mpaka waelewe yaliyomo na kuyafanyia kazi.

Sheikh Othman alisema kama aya hizo zilikuwa na amri, walihakikisha wanazitekeleza, na kama zilikuwa na makatazo, walijitahidi kuyaacha.

Alitoa mfano wa swahaba mtukufu, Omar bin Khattab, ambaye alitumia miaka kadhaa kujifunza Surat Al-Baqarah si kwa sababu ya ugumu wa kuhifadhi, bali kwa kutaka kuelewa na kuishi mafundisho yake.

Sheikh alisema changamoto ya leo ni watu kuipa uzito mkubwa zaidi namna ya kusoma Qur'an kuliko namna ya kuishi kwa mujibu wake.

Alisisitiza kuwa lengo la Qur'an si kutamka herufi zake kwa usahihi pekee, bali kuifanya iwe mwongozo wa maisha.

Alisema Muislamu anapaswa kusoma Qur'an akiwa na swali la msingi: Mwenyezi Mungu ananiamrisha nini hapa, na ananikataza nini?

Sheikh alihimiza Waislamu kuunganisha usomaji wa Qur'an na matendo yao ya kila siku, akisema hapo ndipo Qur'an inapokuwa chanzo halisi cha uongofu na ongezeko la imani.

## MASJID AL-HARAM



# Sheikh Maher: Uongofu unahitaji kuombwa kila siku

IMAMU na Khatibu wa Msikiti Mkuu wa Makka, Sheikh Dkt. Maher bin Hamad Al-Muaiqly, amewataka Waislamu kushikamana na njia iliyonyooka kwa kufuata Qur'an na Sunnah, akisema uongofu si hatua ambayo mtu akiifikia hahitaji tena kumuomba Allah.

Akitoa khutba ya Ijumaa katika Masjid al-Haram, Makka, Septemba 11, Sheikh Maher alisema ndiyo maana Waislamu husoma katika kila rakaa ya Swala: "Tuongoze katika njia iliyonyooka."

Alisema mwenye kupotea humwomba Allah amrudishe katika njia hiyo, huku ambaye tayari yuko katika njia sahihi akiomba athibitishwe na asipotee.

Kwa mujibu wa Sheikh Maher, njia iliyonyooka ni Uislamu, Qur'an ndiyo mwongozo wake na Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) ndiye aliyebainisha namna ya kuifuata.

Alisema kushikamana na njia hiyo kunajengwa juu ya misingi miwili mikubwa, ambayo ni kumpwekesha Allah katika ibada na kumfuata Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani).

"Uthabiti haupimwi kwa matakwa na matamanio ya mtu, bali kwa kushikamana na Kitabu cha Allah na Sunnah," alisema.

Sheikh Maher pia alieleza kuwa kama Allah alivyoweka njia iliyonyooka katika maisha ya dunia, Siku ya Kiyama kutakuwa na Sirat juu ya Jahannam ambayo watu watapita kwa viwango tofauti kulingana na namna walivyoshikamana na njia ya Allah duniani.

Akifafanua matumizi ya neno "tuongoze" badala ya "niongoze" katika Surat Al-Fatiha, alisema hilo linamfundisha Muislamu kutotafuta uongofu wake binafsi pekee, bali kuwaombea pia Waislamu wengine.

Alisema dini ya Allah huunganisha watu, wakati kufuata matamanio na njia potofu husababisha migawanyiko na fitna.

Sheikh Maher pia alisisitiza kuwa kushikamana na njia iliyonyooka hakumaanishi mtu hatakosea.

Alisema anayekosea anatakiwa kurekebisha kosa lake, aliyemdhulumu mwingine amrudishie haki yake na aliyefanya dhambi atubie kwa Allah. Aliwataka Waislamu kuendelea kumuomba Allah uongofu, uthabiti na msamaha, huku wakijiandaa kwa Siku ya Mwisho.

## MASJID IMAAM BUKHARY, MORO




# Sheikh Dhahabu: Muislamu asipitishe siku bila kujifunza

Waislamu wametakiwa kutenga muda kila siku kujifunza dini, wakionya kuwa ujinga wa mambo ya msingi ya Sheria ya Kiislamu unaweza kumfanya Muislamu kuishi maisha yake bila kutekeleza wajibu alioamrishwa na Mwenyezi Mungu.

Akitoa Khutba ya Ijumaa, Septemba 11, 2026, katika Masjid Imaam Bukhary, Morogoro, Sheikh Juma Dhahabu alisema elimu ya dini ni msingi wa maisha ya Muislamu, kwa kuwa humwezesha kutambua wajibu wake na kuishi kwa kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu.

Sheikh Juma alirejea kauli ya Imam Shafi, akieleza kuwa mtu anayeshindwa kujifunza mambo ya dini ambayo ni wajibu kwake kuyajua anaweza kuendelea kubaki katika ujinga huo maisha yake yote.

Alisema Muislamu hapaswi kuruhusu muda upite bila kuongeza elimu yake ya dini, akiwataka waumini kujitathmini matumizi ya muda wao na kuhakikisha kila siku wanapata fursa ya kujifunza jambo linalohusiana na dini yao.

Kwa mujibu wa Sheikh Juma, hata kupita kwa saa moja bila mtu kujifunza jambo lolote kuhusu dini yake kunapaswa kumfanya ajitafakari iwapo ametumia muda huo kwa manufaa.

Alisisitiza kuwa kujifunza dini si jukumu la masheikh, maulamaa au wanafunzi wa madrasa pekee, bali ni wajibu unaomhusu kila Muislamu kwa kiwango cha mambo anayopaswa kuyajua na kuyatekeleza katika maisha yake.

Sheikh Juma aliwataka Waislamu kuifanya elimu ya dini kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku, wakijifunza hata aya moja, hukumu moja au fundisho moja na kuhakikisha wanaliweka katika vitendo.

Alisema elimu hiyo humsaidia Muislamu kuelewa wajibu wake, kutambua mipaka kati ya halali na haramu na kufanya maamuzi yanayozingatia mafundisho ya dini.

Aliongeza kuwa kutafuta elimu kunahitaji bidii na mwendelezo, akiwataka Waislamu kutotumia muda mwingi katika mambo yasiyowajengea uhusiano bora na dini yao.

Kwa msingi huo, Sheikh Juma alisisitiza kuwa Muislamu anayejifunza dini yake hujiandaa vyema zaidi kutekeleza wajibu wake, kuepuka yaliyokatazwa na kuishi kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu.

NA MWANDISHI WETU

# JKCI, King Salman, wafanikisha upasuaji wa moyo watoto 30






Watoto 16 wenye magonjwa ya moyo wamefanyiwa upasuaji katika kambi maalumu inayoendeshwa na wataalamu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), kwa kushirikiana na wenzao kutoka taasisi ya King Salman Humanitarian Aid and Relief Centre ya nchini Saudi Arabia.

Kambi hiyo maalumu ya siku sita imekusudia kuwafanyia upasuaji wa moyo watoto 30 wenye matatizo ya matundu kwenye moyo, mishipa ya damu iliyopishana, pamoja na mishipa iliyoziba inayopeleka damu kwenye mapafu.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, daktari bingwa wa upasuaji wa moyo kwa watoto wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dkt. Felix Shonyela amesema ushirikiano kati ya JKCI na taasisi ya King Salman kwa kipindi cha miaka 10, umekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza idadi ya watoto wenye magonjwa ya moyo waliofanyiwa upasuaji hapa nchini.

Dkt. Shonyela amesema wazazi na walezi wanapaswa kuwafikisha watoto hospitali mapema pale wanapowagundua kuwa na changamoto za kiafya ili kurahisisha matibabu yao na kupata huduma mapema.

Kwa upande wake. daktari bingwa mshauri wa magonjwa ya moyo kutoka Taasisi ya King Salman Humanitarian Aid and Relief Centre ya nchini Saudi Arabia , Dkt. Aljohara Hamza, amesema timu hiyo ilianza kutoa huduma mara baada ya kuwasili JKCI na katika siku mbili za Jumamosi na Jumapili na imefanikiwa kuwafanyia upasuaji watoto 11.

Dkt. Aljohara amesema taasisi hiyo itaendelea kufanya kazi kwa weledi na kushirikiana na madaktari wa JKCI ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa na watoto wengi zaidi wanapata huduma kupitia kambi hiyo.

"Tumefurahishwa na uwezo wa wataalamu wa JKCI katika kutoa huduma za kibingwa za upasuaji wa moyo kwa watoto,na uwezo wao ni tofauti na tulivyoanza kushirikiana miaka 10 iliyopita", ameseema Dkt. Aljohara.

NA MWANDISHI WETU

# Tanzania yaingia mjadala wa AI na mustakabali wa vyuo vikuu Afrika

**Akili bandia (AI) imeingia rasmi kwenye ajenda ya vyuo vikuu Afrika, huku Tanzania ikiwa mwenyeji wa mjadala unaolenga kuamua namna wahitimu watakavyokabiliana na ajira, utafiti na teknolojia inayobadili dunia.**

Vyuo vikuu barani Afrika vinakabiliwa na mjadala mpya kuhusu namna ya kuandaa wahitimu, kubadili mifumo ya ufundishaji na kuimarisha utafiti katika dunia inayobadilishwa kwa kasi na akili bandia (AI).

Mjadala huo utakuwa miongoni mwa ajenda kuu za viongozi wa elimu ya juu watakaokutana Dar es Salaam kuanzia Septemba 16 hadi 22, 2026, katika Mkutano wa Mwaka wa 2026 wa Alliance for African Partnership (AAP).

Mkutano huo unaandaliwa kwa pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Michigan State University, ukiwa na kaulimbiu "Kufikiria Upya Elimu ya Juu kwa Mustakabali wa Afrika: Uongozi, Ubunifu na Ushirikiano wa Kimataifa."

Utawakutanisha viongozi wa vyuo vikuu, wasomi, watunga sera, wabunifu, wawakilishi wa sekta binafsi na wadau wa maendeleo kutoka Afrika na nje ya bara hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari Septemba 14, 2026, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anayeshughulikia Utafiti, Profesa Nelson Boniface, alisema mkutano huo unatoa fursa kwa taasisi za Afrika kujadili changamoto na fursa zinazoikabili sekta ya elimu ya juu.

"Mustakabali wa Afrika kwa sehemu unategemea uwezo wa vyuo vyetu kuunganisha maarifa na changamoto pamoja na fursa zinazokabili jamii zetu," alisema.

Kauli hiyo inaweka mjadala wa AI ndani ya changamoto pana inayovikabili vyuo vikuu Tanzania—kuhakikisha maarifa yanayozalishwa kwenye madarasa na maabara za utafiti yanageuka kuwa suluhisho lenye manufaa kwa jamii na uchumi.

## AI na ajira

Mkutano huo utakuwa na mjadala maalumu wa umma Septemba 17 kuhusu "AI na Mustakabali wa Ajira", utakaowakutanisha wadau wa elimu ya juu, teknolojia na sekta binafsi kujadili namna wahitimu watakavyoweza kutumia teknolojia hiyo kwa uwajibikaji.

Mjadala huo unafanyika wakati AI inaanza kubadili aina ya ujuzi unaohitajika na waajiri, namna taarifa zinavyozalishwa na kupatikana, pamoja na jinsi wanafunzi wanavyofanya kazi za kitaaluma.

Vyuo hivyo sasa vinakabiliwa na jukumu la kuwaandaa wahitimu wasioishia kujua kutumia zana za AI, bali pia kuelewa mipaka yake, kuitumia kwa maadili na kuhifadhi ujuzi wa kibinadamu unaohitajika katika mazingira ya kazi.

Teknolojia hiyo pia imeibua maswali mazito ndani ya taaluma, ikiwamo namna vyuo vinavyopaswa kushughulikia kazi zinazozalishwa na AI, kiwango ambacho wanafunzi wanapaswa kuruhusiwa kutumia AI katika utafiti na uandishi wa kitaaluma, pamoja na namna wakufunzi watakavyopima uelewa halisi wa mwanafunzi wakati teknolojia inaweza kutoa majibu ya kiwango cha juu ndani ya sekunde.

Masuala hayo yanazidi kuwa muhimu wakati Tanzania ikijenga uchumi unaotegemea zaidi teknolojia, ubunifu na maarifa.

## Utafiti kwenda kwa jamii

Hata hivyo, mjadala wa AAP hautahusu AI pekee. Mkutano huo utajadili namna vyuo vikuu vinavyoweza kuimarisha uongozi wa umma, kuwaandaa wahitimu kwa mabadiliko ya ajira, kukuza utafiti na ubunifu na kujenga ushirikiano wenye matokeo kwa jamii.

Katika Innovation Forum, vyuo vikuu, wajasiriamali, wawekezaji na viongozi wa sekta binafsi watajadili namna utafiti na maarifa yanavyoweza kubadilishwa kuwa suluhisho, biashara na manufaa kwa jamii.

Profesa Boniface alisema mkutano huo utatoa nafasi ya kutafakari namna utafiti, ubunifu, uongozi na ushirikiano wa kimataifa vinavyoweza kuleta suluhisho la vitendo na matokeo ya kudumu.

AAP ni mtandao unaoongozwa na vyuo vikuu na unaoratibiwa na Michigan State University, ukiwa na taasisi 12 kutoka nchi 10 za Afrika, zikiwamo Tanzania, Uganda, Kenya, Malawi, Afrika Kusini, Botswana, Zimbabwe, Mali, Senegal na Nigeria.




**Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) anayeshughulikia Utafiti, Profesa Nelson Boniface, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu Mkutano wa Mwaka wa 2026 wa Alliance for African Partnership (AAP), utakaofanyika UDSM kuanzia Septemba 16 hadi 22. Mkutano huo utajadili nafasi ya vyuo vikuu katika enzi ya akili bandia (AI).**

UKHTI FATIMA SS




# Kenya yatakiwa kubadili kanuni kukuza benki za Kiislamu

KENYA imetakiwa kufanya mageuzi ya haraka ya kanuni ili kufungua fursa zaidi katika sekta ya benki na fedha za Kiislamu, ambayo wataalamu wanasema bado haijatumia kikamilifu uwezo wake.

Kwa mujibu wa Eastleigh Voice, wadau waliozungumza katika Islamic Banking Forum and Dialogue mjini Nairobi Septemba 10 walisema mapungufu ya kisheria na uratibu dhaifu wa sera yanazuia ubunifu wa bidhaa mpya za kifedha.

Wadau hao walisema taasisi za fedha za Kiislamu bado zinafanya kazi kwa kiwango kikubwa chini ya sheria za kawaida kupitia misamaha maalumu, hali inayofanya mfumo kuwa mgumu na usio na mwongozo mmoja wa fedha za Kiislamu.

Miongoni mwa maeneo yaliyotajwa kuwa na fursa ni sukuk, takaful, benki za rejareja, fedha za kijani na ufadhili wa biashara ndogo.

Kwa mujibu wa Eastleigh Voice, washiriki pia walitaka serikali kuongeza matumizi ya sukuk za serikali na kampuni ili kuvutia mitaji na kutoa maeneo salama ya uwekezaji kwa taasisi zinazofuata Shariah.

Wadau walieleza kuwa soko la wananchi wa kawaida bado halijatumika vizuri kutokana na uelewa mdogo wa bidhaa za Kiislamu.

Pia walipendekeza matumizi ya sukuk za kijani kusaidia Kenya kukusanya sehemu ya takribani dola bilioni 62 zinazohitajika kwa hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hadi mwaka 2030.

## Fitch yatwaa tuzo ya kimataifa katika fedha za Kiislamu

**FITCH Ratings imetwaa Tuzo ya Global Islamic Finance Awards (GIFA) 2026 katika kipengele cha tathmini za fedha za Kiislamu, ikiwa ni mwaka wa saba mfululizo taasisi hiyo kutambuliwa na tuzo hizo.**

**Mkuu wa Fedha za Kiislamu wa Fitch, Bashar Al-Natoor, naye ametajwa kuwa Mtaalamu Bora wa Mwaka 2026 katika tathmini na upangaji wa fedha za Kiislamu. Fitch imesema tuzo hizo zinaakisi nafasi yake katika kutoa tathmini za mikopo, tafiti na uchambuzi unaosaidia kuongeza uwazi na kufanya maamuzi katika sekta ya fedha za Kiislamu.**

**Kwa sasa, Fitch inatoa tathmini kwa zaidi ya asilimia 72 ya sukuk zote za kimataifa zinazotolewa kwa dola za Marekani. Hadi mwisho wa nusu ya kwanza ya mwaka 2026, sukuk zilizotathminiwa na Fitch zilikuwa na thamani ya dola bilioni 238, zikihusisha zaidi ya hati 310 na programu zaidi ya 100 za sukuk.**

## Amana za benki za Kiislamu Afrika Kusini zakua asilimia 151

**AMANA za wateja katika benki za Kiislamu nchini Afrika Kusini zimeongezeka kwa asilimia 151 ndani ya miaka mitano, zikionyesha ukuaji wa kasi wa huduma za fedha zinazofuata misingi ya Shariah.**

**Kwa mujibu wa makala ya Moneyweb iliyoandikwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Banking Association South Africa (Basa), Bongiwe Kunene, amana hizo ziliongezeka kutoka randi bilioni 43.3 Desemba 2020 hadi randi bilioni 108.7 Desemba 2025.**

**Katika kipindi hicho, mali za ufadhili wa Kiislamu ziliongezeka kutoka randi bilioni 16.9 hadi bilioni 25.7.**

**Kunene amesema benki za Kiislamu zimeendelea kuwa sehemu inayotambulika katika mfumo wa fedha wa Afrika Kusini, ingawa bado ni ndogo ikilinganishwa na benki za kawaida.**

## Uwekezaji wa Ghuba wachochea fedha za Kiislamu Misri

**MISRI inatarajiwa kushuhudia ukuaji zaidi wa sekta ya fedha za Kiislamu katika nusu ya pili ya 2026 na mwaka 2027, ukichochewa na uwekezaji kutoka nchi za Ghuba, mageuzi ya kanuni na mahitaji ya vyanzo mbadala vya fedha.**

**Kwa mujibu wa Fitch Ratings, thamani ya sekta ya fedha za Kiislamu nchini humo ilizidi dola bilioni 40 mwishoni mwa nusu ya kwanza ya 2026. Misri pia ndiyo soko kubwa zaidi la sukuk barani Afrika.**

**Sukuk zilizokuwa sokoni zilifikia dola bilioni 3.5, ongezeko la takribani asilimia 40 kwa mwaka mmoja. Nchi hiyo pia ilikuwa na ufadhili wa pamoja wa Kiislamu wenye thamani ya dola bilioni 16.**

**Misri ina benki nne kamili za Kiislamu zenye mali inayozidi dola bilioni 18.6, huku benki nyingine 11 za kawaida zikitoa huduma za Kiislamu.**

## Maldives yajielekeza kwenye utalii wa halal

**MALDIVES imeanza mkakati wa kuifanya halal tourism kuwa sehemu maalumu ya sekta yake ya utalii, ikilenga kuvutia zaidi wasafiri Waislamu kutoka maeneo mbalimbali duniani.**

**Kuelekea lengo hilo, Ofisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji wa Visit Maldives Corporation (VMC), Abdulla Yasir alikutana na Katibu Mkuu wa Islamic Chamber of Commerce and Development, Sheikh Yousef Hasan Khalawi, kujadili bidhaa za utalii wa halal, uthibitishaji na huduma maalumu kwa wasafiri Waislamu, inaripoti tovuti yaTravelMole,**

**Hatua hiyo inaunga mkono msukumo wa Rais Mohamed Muizzu wa kuifanya halal tourism kuwa sehemu rasmi ya mkakati wa kitaifa wa utalii.**

**Mwaka 2025, Maldives ilipokea watalii zaidi ya milioni 2.24. Kati yao, zaidi ya 210,000 walitoka katika masoko 19 yenye idadi kubwa ya Waislamu, ikiwamo Saudi Arabia, UAE, Uturuki, Malaysia, Pakistan, Indonesia na Qatar.**

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Wafadhili wa misikiti hili liangalieni upya

**Kwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na kasi kubwa ya ujenzi wa misikiti katika maeneo mbalimbali. Ni jambo la kujivunia kuona watu binafsi, familia, vikundi, taasisi na wafadhili mbalimbali wakijitokeza kwa moyo wa kujitolea kujenga nyumba za ibada kwa ajili ya Waislamu.**

**Wengine wamejenga misikiti katika maeneo ambayo hapo awali waumini walilazimika kusafiri umbali mrefu kutafuta sehemu ya kuswali, huku wengine wakigharamia ukarabati, upanuzi na uendeshaji wa misikiti hiyo. Hii ni kazi yenye thamani kubwa na inastahili pongezi.**

**Kwa hakika, wafadhili wa misikiti wana malipo makubwa kwa kuiwezesha jamii kupata maeneo mazuri na salama ya ibada.**

**Mtu anayetoa fedha kujenga msikiti, kununua vifaa, kulipia huduma mbalimbali au kugharamia shughuli za msikiti, anafanya jambo lenye manufaa makubwa kwa jamii.**

**Wafadhili wengi wameonyesha moyo wa hali ya juu wa kujitolea, na juhudi zao zimewezesha misikiti mingi kujengwa kwa kasi na kuanza kutumika ndani ya muda mfupi.**

## Tatizo liko hapa

Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, kuna jambo ambalo wafadhili wa misikiti wanapaswa kulitafakari kwa kina. Misikiti mingi inayojengwa na kuendeshwa na wafadhili ambao hawaruhusu kabisa michango kutoka kwa waumini, hukumbwa na changamoto fulani katika uendeshaji wake.

Tatizo si kwamba wafadhili hawasaidii; tatizo linaweza kutokea pale msaada huo unapofanya waumini wajione kana kwamba hawana nafasi yoyote katika kushughulikia mahitaji ya msikiti wao.

Msikiti ni nyumba ya ibada, lakini pia ni sehemu ambayo waumini hukutana mara kwa mara na kujenga uhusiano wa kijamii. Kwa hiyo, waumini wanapaswa kuhisi kuwa ni sehemu ya msikiti wanaousalia, hata kama ujenzi wake au gharama zake kubwa zilifanywa na wengine.

Hapa ndipo umuhimu wa kuwashirikisha waumini unapojitokeza.

Kwa mfano, msikitini kunaweza kutokea changamoto ndogo kama kuharibika kwa taa, bomba la maji, feni, mfumo wa sauti, sehemu ya kutawadhia au hitilafu nyingine inayohitaji fedha kidogo tu kurekebishwa.

Kwa kawaida, waumini wanaweza kuchanga kiasi kidogo na tatizo hilo likamalizika ndani ya muda mfupi. Lakini inapokuwa msikiti una "wenyewe" kwa maana ya wafadhili ambao wameweka utaratibu kwamba waumini hawaruhusiwi kuchangia, jambo dogo linaweza kubaki kwa muda mrefu bila kutatuliwa.

Hali huwa mbaya zaidi pale changamoto hiyo inapoanza kuhusishwa na urasimu wa wafadhili.

Huenda waumini wakaambiwa taarifa itatumwa kwa mfadhili, kisha kusubiri majibu, kuomba fedha, kusubiri idhini na hatimaye kusubiri utekelezaji.

Mchakato huo unaweza kuchukua wiki au hata miezi, wakati tatizo lenyewe linaweza kuwachukua waumini siku moja kulitatua mara moja kwa mchango wao.

Hapa ndipo tunapopaswa kujiuliza: Je, kusimamia msikiti kunapaswa kusababisha kero kwa waumini wanaokuja kuswali?

Jibu ni hapana. Ufadhili unapaswa kuwa chanzo cha wepesi wa ibada, si sababu ya kuongezeka kwa usumbufu.

Ikiwa mfadhili amejenga msikiti kwa nia njema, ni muhimu pia kuhakikisha mfumo wa uendeshaji unawapa waumini nafasi ya kushiriki katika kutatua changamoto ndogo ndogo zinazojitokeza.

Ni jambo zuri mfadhili kutaka kuhakikisha fedha zinatumika kwa uwazi na kwa malengo yaliyokusudiwa. Lakini uwajibikaji haupaswi kugeuka kuwa urasimu unaozuia suluhisho la hata matatizo madogo.

Inawezekana kuwepo kwa utaratibu mzuri wa usimamizi unaowezesha waumini kuchangia na kutumia fedha hizo kwa mahitaji madogo chini ya usimamizi wa kamati ya msikiti, huku matumizi makubwa yakiendelea kuhitaji idhini ya mfadhili.

Wafadhili wanapaswa pia kuelewa kuwa kuwashirikisha waumini hakupunguzi heshima yao wala thamani ya mchango wao.

Badala yake, kunajenga umiliki wa pamoja, uwajibikaji na upendo kwa msikiti.

Muumini anayejua kwamba anaweza kusaidia kununua taa iliyoharibika, kurekebisha bomba au kusaidia huduma nyingine ndogo, atahisi kuwa msikiti ni sehemu yake na atakuwa tayari kuutunza.

Ni wakati sasa wafadhili wa misikiti wakapitia upya mifumo ya uendeshaji wa misikiti yao. Lengo liwe kuhakikisha kwamba msaada wao unaendelea kuwa baraka, huku waumini wakipewa nafasi ya kushiriki pale inapohitajika. Changamoto zitatuliwe haraka, hasa zile ndogo ambazo hazihitaji taratibu ndefu za kiofisi.

Kwa wafadhili, pongezi kubwa kwa kazi mnayoifanya ya kujenga na kuiendesha misikiti. Lakini dhima yenu haishii kwenye kujenga kuta na kuweka paa. Dhima yenu pia ni kuhakikisha nyumba hizo za ibada zinaendeshwa kwa namna inayowapa waumini urahisi, heshima na utulivu wakati wa ibada.

Msikiti usiwe chanzo cha kero kwa anayekuja kuswali. Uwe mahali pa utulivu, ibada na mshikamano.

Wafadhili mna dhima kubwa; simamieni misikiti kwa moyo wa huduma, lakini pia waruhusuni waumini kuwa sehemu ya suluhisho. Changamoto zitatuliwe haraka.

NA UKHTI FATIMA



# Una uwezo wa kununua gari, lakini je una uwezo wa kulimiliki?

**WATU wengi wanapopanga kununua gari huanza na swali moja: Bei yake ni kiasi gani? Lakini hilo si swali muhimu zaidi.**

**Swali kubwa ni: Baada ya kulinunua, unaweza kulihudumia bila kuvuruga maisha yako ya kifedha?**

**Unaweza kuwa na Sh milioni 15 au 20 taslimu na ukafanikiwa kununua gari. Lakini hapo gharama hazijaisha. Kwa kweli, hapo ndipo gharama za umiliki zinaanza.**

**Vyanzo vya elimu ya fedha kuhusu magari vinaonya kwamba bei ya ununuzi ni sehemu moja tu ya gharama. Baada yake kuna mafuta, bima, matengenezo, usajili, matairi, marekebisho na wakati mwingine riba ya mkopo. Kwa hiyo, kuwa na uwezo wa kununua gari si sawa na kuwa na uwezo wa kulimiliki.**

## Mafuta: Gharama inayokuja kila wiki

Kabla hujanunua gari, jiulize utakuwa unalitumia kiasi gani. Mtu anayesafiri kilomita chache kwa siku ana gharama tofauti na anayesafiri kutoka mbali kwenda kazini kila siku.

Aina ya injini, ukubwa wa gari, foleni na namna unavyoendesha vyote vinaathiri matumizi ya mafuta. Hivyo usinunue gari kubwa kwa sababu tu linavutia halafu kila mwisho wa wiki mafuta yanakuwa tatizo.

Wakati mwingine gari dogo, linalotumia mafuta kidogo, linaweza kuwa uamuzi bora zaidi wa kifedha kuliko gari kubwa linalokupa hadhi lakini linakula sehemu kubwa ya kipato chako.

## Huduma na matengenezo havina likizo

Gari linahitaji mafuta ya injini, chujio (filters), ganda za breki (brake pads), matairi, betri, matairi na vipuri vingine. Na haya si mambo ya "ikiwa yatatokea." Baadhi yake lazima yatokee kadri gari linavyotumika.

Tatizo ni kwamba watu wengi hununua gari wakifikiria bei ya gari pekee na hawatenge fedha ya matengenezo. Matokeo yake, muda wa matengenezo (service0 ukifika wanaahirisha. Sauti mpya inapotokea kwenye injini wanaongeza redio. Tatizo dogo linageuka kuwa tatizo kubwa na gharama zinaongezeka.

Matengenezo ya kawaida yanaweza kusaidia kuzuia hitilafu ndogo zisigeuke kuwa marekebisho makubwa na ya gharama zaidi.

## Usisahau bima, leseni na gharama za pembeni

Kuna gharama ambazo hazionekani kila siku lakini lazima uzihesabu. Bima. Ada na leseni zinazohitajika. Maegesho. Ushuru au tozo zinazohusika. Kuosha gari. Ulinzi. Matairi. Kisha kuna zile zinazokuja bila taarifa. Betri imekufa. Tairi limepasuka. Gari limegongwa. Kioo kimevunjika. Mfumo fulani umeharibika.

Chanzo kimoja cha gharama za umiliki kinaonya kuwa hata gharama za tozo za maegesho na matengenezo zisizotarajiwa ni sehemu ya gharama halisi ya kuwa na gari. Kwa hiyo bajeti ya gari lazima iwe na nafasi ya dharura.

## Gari nalo linapoteza thamani

Kuna gharama ambayo watu wengi hawaioni kwa sababu hailipwi dukani: kupungua kwa thamani ya gari. Ukinunua gari leo kwa kiasi fulani, baada ya miaka kadhaa huenda lisiweze kuuzwa kwa bei ileile.Tofauti hiyo nayo ni gharama.

Kwa magari mapya, kupungua kwa thamani kunaweza kuwa sehemu kubwa ya gharama ya muda mrefu ya umiliki.

Ndiyo maana wakati mwingine kununua gari lililotumika vizuri kunaweza kuwa na maana zaidi kuliko jipya, hasa kama lengo lako ni usafiri na si kujionyesha.

## Mkopo unaweza kufanya gari liwe ghali zaidi

Kwa vyovyote, kamwe kamwe usichukue gari kwa mkopo wa riba kwani hilo ni haramu isiyo na mjadala katika dini na gharama yake kiroho ni kubwa zaidi mbele za Allah Mtukufu.

Njia mbadala ni kwenda katika taasisi za kifedha za Kiislamu uone kama kuna bidhaa kama hiyo ya kukunulia gari na kuwalipan kwa awamu pamoja na faida. Ikiwa hivyo pia,, usiangalie awamu za malipo za kila mwezi pekee. Angalia pia kiasi utakacholipa mpaka mwisho, pamoja na faida mliyokubaliana. Faida unayomlipa aliyekukopesha kwa makubaliano ya miamala ya Kiislamu inaweza kufanya gari ulilodhani linagharimu kiasi fulani likugharimu zaidi sana.

Jiulize pia: Nikikosa kipato kwa miezi miwili au mitatu, bado nitaweza kulipa awamu za marejesho na kuendesha gari? Kama jibu ni hapana, huenda umejinyoosha zaidi ya uwezo wako.

## Unawezaje kupunguza gharama?


Anza kwa kuchagua gari linaloendana na maisha yako, si matarajio ya watu. Fanya matengenezo kwa wakati. Endesha kwa utulivu; kuongeza kasi ghafla, kukanyaga breki mara kwa mara na kuacha injini ikiendelea bila sababu huongeza matumizi ya mafuta na uchakavu.

Pia tafuta gari lenye vipuri vinavyopatikana, mafundi wanaolijua na matumizi ya mafuta unayoweza kuyamudu. Muhimu zaidi, kabla hujanunua, tengeneza bajeti ya mwezi ya gari zima, si bei ya mafuta pekee. Mwisho wa yote, gari linapaswa kurahisisha maisha yako.

Likianza kula akiba, kukusukuma kwenye madeni na kukufanya uogope kila taa ya dashboard inapowaka, huenda halijakupa uhuru ulioutafuta.

SEHEMU YA 1

# Ukosefu wa uaminifu katika utawala wa Waqf Tanzania: Tatizo liko wapi?



**Waqf ni miongoni mwa taasisi kongwe na zenye nguvu katika historia ya Uislamu. Kwa karne nyingi, Waqf imekuwa msingi wa ujenzi wa misikiti, madrasa, shule, vituo vya afya, visima vya maji na huduma nyingine za kijamii.**

Nchini Tanzania, historia ya Waqf ina mizizi ya kina, husussan katika maeneo ya Pwani na Zanzibar. Hata hivyo, pamoja na umuhimu huo, sekta ya Waqf inakabiliwa na changamoto ambayo haionekani kwa macho, lakini ina athari kubwa: upungufu wa uaminifu (Trust Deficit) kati ya baadhi ya wafadhili na jamii kwa upande mmoja, na mifumo ya usimamizi wa Waqf kwa upande mwingine.

Swali muhimu ni: Kwa nini baadhi ya Waislamu wenye uwezo mkubwa wa kifedha leo hawako tayari kuweka mali zao wakfu?

Moja ya majibu muhimu ni kutokuwa na imani ya kutosha kwamba mali zao zitasimamiwa kwa uwazi, weledi na uadilifu.

## Kwanza: ukosefu wa uwazi

Jamii mara nyingi huhitaji kujua mali za Waqf zilipo, zina thamani gani, zinazalisha kiasi gani na mapato yake yanatumika wapi. Taarifa hizi zisipopatikana kwa uwazi, huibua mashaka.

Katika utawala wa kisasa, uwazi ni msingi wa uaminifu. Taarifa za kifedha zinazotayarishwa vizuri na kukaguliwa na wataalamu huru zinaweza kusaidia kuondoa mashaka na kujenga imani.

## Pili: Mali za Waqf kudorora

Tatizo jingine ni kuwepo kwa mali za Waqf ambazo hazitumiki kwa ufanisi au zimeachwa zikidhoofika.

Nyumba, maduka, maghala au viwanja visipotunzwa na kuendelezwa, si mapato pekee yanayopotea; hata imani ya jamii huathirika. Mtu anapoona mali iliyowekwa wakfu na waliomtangulia imetelekezwa, anaweza kusita kuiweka mali yake mwenyewe katika mfumo huo.

## Tatu: Mapato kutotoa matokeo yanayoonekana

Waqf inalenga kuzalisha manufaa kwa walengwa. Ikiwa mapato ya nyumba, maduka au mali nyingine hayatoi matokeo yanayoonekana katika elimu, afya, kusaidia maskini, mayatima na vijana, jamii huanza kujiuliza: Mapato haya yanaenda wapi? Hili linaweza kugeuza Waqf kutoka kuwa chombo cha maendeleo ya jamii na kuonekana kama mfumo wa kudumisha taasisi zinazousimamia.

## Nne: Uingiliaji wa kisiasa na ukosefu wa utaalamu

Waqf inahitaji uongozi wenye uadilifu na utaalamu. Pale ambapo uteuzi wa viongozi unatokana zaidi na siasa, makundi au mahusiano kuliko uwezo, ufanisi wa Waqf unaweza kudhoofika.

Waqf ya kisasa inahitaji pamoja na ucha Mungu, wataalamu wa uhasibu, uwekezaji, usimamizi wa mali, sheria, uchumi na teknolojia, wakishirikiana na wataalamu wa Shariah.

## Athari ni kubwa

Athari kubwa ya Trust Deficit ni kudhoofika kwa utamaduni wa Sadaqah Jariyah kupitia Waqf. Watu wenye uwezo wanaweza kuchagua kubaki na mali zao chini ya udhibiti binafsi badala ya kuziingiza katika mfumo wa Waqf.

Matokeo yake ni kupungua kwa mali mpya za Waqf, kudhoofika kwa huduma za kijamii na kuongezeka kwa hatari ya mali zilizopo kupoteza thamani au kuvamiwa.

Kwa hiyo, tatizo si Waqf yenyewe. Tatizo ni namna tunavyoiendesha. Ikiwa tunataka Waqf irejee kuwa injini ya maendeleo ya jamii, tunahitaji kujenga upya kitu kimoja muhimu: uaminifu na uadilifu.

Na swali linalofuata ni: Tunawezaje kujenga upya uaminifu huo?

Fuatilia Makala yetu inayofuata: Kujenga Upya Uaminifu: Jinsi ya Kuifanya Waqf Tanzania Kuwa Injini ya Maendeleo

NA Mahmoud Nyamguma

# Nchi 8 za Kiislamu zataka hatua kali dhidi ya Israel



Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia, UAE, Qatar, Misri, Jordan, Indonesia, Pakistan na Uturuki wameungana kuishinikiza jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua zaidi dhidi ya biashara na huduma zinazohusishwa na makazi ya Israel katika maeneo ya Palestina yanayokaliwa kimabavu.

Nchi hizo nane pia zimesisitiza suluhu ya mataifa mawili, likiwemo taifa huru la Palestina lenye mipaka ya kabla ya 4 Juni 1967 na Jerusalem Mashariki kuwa mji mkuu.

Kauli hiyo inakuja wakati Uingereza imetangaza kupiga marufuku uagizaji wa bidhaa kutoka katika makazi hayo na kuweka vikwazo kwa baadhi ya huduma zinazohusiana nayo.

Ufaransa na Canada pia zimechukua au kutangaza hatua dhidi ya bidhaa kutoka kwenye makazi hayo, huku nchi nyingine za Ulaya zikijadili vikwazo zaidi.

Ikumbukwe pia kuwa Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) katika shauri lake la Julai 2024 ilisema makazi ya Israel katika Ukingo wa Magharibi na Jerusalem Mashariki yameanzishwa na kudumishwa kinyume cha sheria za kimataifa, huku ikiitaka Israel kusitisha mara moja shughuli mpya za ujenzi wa makazi.

Hata hivyo, athari za moja kwa moja za vikwazo hivyo kwa kibiashara zinaweza kuwa ndogo kutokana na ukubwa wa mauzo ya bidhaa hizo; hivyo, uzito mkubwa wa hatua hizi ni ujumbe wa kisiasa na kisheria kwamba biashara haiwezi kutenganishwa na namna ardhi inavyotwaliwa na makazi yanavyopanuliwa.

Israel imepinga vikali hatua hizo na kujibu kwa hatua za kidiplomasia dhidi ya Uingereza.

ikiwa makazi yanaendelea kupanuka huku dunia ikisema yanakiuka sheria za kimataifa, je, jumuiya ya kimataifa inaweza kulinda haki ya Wapalestina ya kujitawala na kupatikana kwa suluhu ya mataifa mawili kwa kauli pekee, au inapaswa kugeuza shinikizo la kidiplomasia kuwa hatua halisi za kiuchumi na kisheria?

NA Mahmoud Nyamguma

# Mahakama India yabomoa msikiti kutanua barabara ya Hija ya Wahindu

Mahakama Kuu ya Madhya Pradesh nchini India imeondoa kizuizi cha kisheria kilicholinda sehemu ya eneo la Shahi Masjid, msikiti wa takribani karne moja mjini Ujjain kubomolewa ili kupanua barabara kwa ajili ya maandalizi ya Simhastha Kumbh 2028, hija kubwa ya Kihindu.

Mahakama imesema hatua hiyo inalenga usalama wa umma, usimamizi wa msongamano na kuwahudumia mamilioni ya mahujaji, huku maswali yakizuka kuhusu uwiano kati ya maendeleo ya miundombinu na ulinzi wa maeneo ya ibada ya Waislamu.

Barabara hiyo inayopakana na msikiti inapangwa kufikia upana wa mita 15, hivyo kulazimu kuodnoa takribani mita za mraba 39.33 za msikiti.

Wasimamizi wa msikiti, ambao ni mali iliyosajiliwa kama Waqf, walipinga wakisema inagusa maeneo ya matumizi ya waumini, ikiwemo sehemu ya Jamat Khana na miundombinu mingine ya msikiti. Mahakama, hata hivyo, ilikataa hoja za ukiukwaji wa haki za kikatiba za usawa na uhuru wa dini, ikisisitiza "maslahi mapana ya umma."

Suala hili si tu la barabara bali ni mtihani wa namna India inavyolinda uhuru wa dini, urithi wa kihistoria na usawa wa raia wakati ikiandaa matukio makubwa ya kidini.

Ikiwa miundombinu ya hija ya Kihindu inahitaji kubadilisha sehemu ya msikiti wa Waislamu, hoja ya msingi kwa watunga sera je maendeleo hayo ya upanuzi yasingeweza kufanyika bila kuumiza jamii za wachache, kama Waislamu?

## Rais Mwinyi ataka uwekezaji uguse maisha ya wananchi

**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema wananchi wanapaswa kupewa kipaumbele katika ajira na fursa zinazotokana na uwekezaji, akisisitiza kuwa uwekezaji haupaswi kuishia katika ujenzi wa majengo.**

**Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga katika uzinduzi wa hoteli mpya ya kisasa katika kijiji cha Jambiani, Mkoa wa Kusini Unguja, Dkt Mwinyi alisema uwekezaji unapaswa kugusa maisha ya wananchi na usiishie kwenye uwepo wa majengo mazuri tu.**

**Hoteli hiyo iliyogharimu Dola za Marekani milioni 6.5, sawa na takribani Sh17 bilioni, imejengwa na kampuni ya Jude Zanzibar Holding Company ya nchini Misri, ikiwa ni sehemu ya matokeo ya ushirikiano wa kidiplomasia na kiuchumi kati ya Zanzibar na Jamhuri ya Kiarabu ya Misri.**

**Katika hotuba hiyo, Dkt. Mwinyi alipongeza kampuni hiyo kwa kuajiri wazawa 85 kati ya wafanyakazi 90, hivyo kuendana na azma ya Serikali ya kuhakikisha wananchi ni wanufaika wakuu wa uwekezaji huku fursa za soko kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati, wakulima, wasafirishaji na wasanii pia zikifunguka.**

**Dkt. Mwinyi alisema ongezeko la uwekezaji linaendana na ukuaji wa utalii Zanzibar, akibainisha kuwa mwaka 2025 visiwa hivyo vilipokea watalii 917,167, sawa na ongezeko la asilimia 24.5 ikilinganishwa na mwaka 2024.**

## Sheikh aelekeza: Msijimilikishe vitu mlivyookota

**JAMII imetakiwa kuepuka kujimilikisha vitu ilivyookota bila kufanya juhudi za kumtafuta mwenye mali hiyo.**

**Sheikh Mwinyimvua Omary, akizungumza wilayani Bagamoyo, amesema kurejesha mali iliyopotea kwa mwenyewe ni sehemu ya uaminifu na jambo lenye malipo mema mbele ya Mwenyezi Mungu.**

**Alisema anayepata kitu kilichopotea anapaswa kutumia njia mbalimbali kumtafuta mwenyewe, ikiwamo kutoa taarifa kupitia viongozi wa dini, Serikali na mitandao ya kijamii.**

**Sheikh Omary ali9shauri kuwa wakati wa kutangaza kitu kilichookotwa, baadhi ya alama zake muhimu zisielezwe ili zitumike kumtambua mmiliki halisi atakapojitokeza.**

**Aliongeza kuwa taratibu za Kiislamu kuhusu mali iliyookotwa zinapaswa kufuatwa kulingana na thamani na muda uliopita bila mwenyewe kujitokeza, huku akisisitiza kuwa nia kuu iwe kuhifadhi amana na kuirejesha kwa mwenye haki.**

**Katika hatua nyingine, Sheikh huyo ametakiwa wazazi kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi na kukua katika mazingira salama na yenye maadili.**

**Alisema wazazi wana wajibu wa kuwalea na kuwaongoza, badala ya kuwaacha wajitegemee katika umri ambao bado wanahitaji uangalizi huku pia akikiri kuwa malezi bora yana mchango mkubwa katika kujenga kizazi chenye maadili, utii, uaminifu na bidii, ambacho kitakuwa na manufaa kwa familia, jamii na Taifa.**

## DC Bagamoyo aipa Sirajulmunir simenti mifuko 50

**Mkuu wa wilaya ya Bagamoyo, Shaibu amechangia mifuko 50 ya simenti kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula katika shule ya Msingi Sirajulmunir iliyopo kata ya Nianjema wilayni Bagamoyo.**

**Akiwakilishwa na Ibrahim Gama katika mahafali ya 16 ya wahitimu wa darasa la saba shuleni hapo, , Ndemanga alisema juhudi za shule hiyo zinapaswa kuungwa mkono na kila mpenda maendeleo ndani na nje ya Bagamoyo na kwamba anaunga mkono wazo la kuanzishwa kwa shule ya dada ya Sekondari ili wahitimu waende katika Sekondari yao ya Sirajulmunir.**

**Shule hiyo inayomilikiwa na Sirajulmunir Islamic Centre, ni moja ya shule zinazofanya vizuri zaidi katika mitihani ya kitaifa kwa Bagamoyo huku wahitimu wake pia wakisifika kwa maadili mema**

**Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Amiri wa Taasisi ya Sirajulmunir Islamic Centre, Sheikh Abdallah Kindamba, ametoa wito kwa wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao katika shule za Kiislamu ili wapate elimu bora sambamba na malezi sahihi yatakayowajengea hofu ya Mungu na uadilifu na hatimaye kuwa raia bora.**

NA Mahmoud Nyamguma

# Licha ya chuki; Uislamu umeimarika Marekani miaka 25 baada ya 9/11,



Miaka 25 baada ya mashambulizi ya Septemba 11, 2001, Waislamu nchini Marekani wameendelea kukabili ubaguzi na kauli za chuki, lakini wakati huo huo wameongeza ushiriki wao katika siasa, elimu na maisha ya kiraiam tovuti ya  The Gurdian ya Uingereza imeripoti.

Utafiti wa Pew Research Center wa 2026 unaonyesha kuwa asilimia 59 ya Waislamu Marekani wanasema kuna ubaguzi mkubwa dhidi yao, huku asilimia 59 pia wakisema taswira ya Waislamu katika vyombo vya habari si ya haki.

Hata hivyo, mazingira hayo hayajawazuia Waislamu kujenga taasisi na nafasi zao.

Takwimu mpya kuna viongozi Waislamu 255 waliochaguliwa katika majimbo 26 ya Marekani, wakiwemo wabunge, majaji na mameya.

New York pia imeshuhudia kuapishwa kwa Zohran Mamdani kuwa meya wa kwanza Muislamu wa jiji hilo misikiti nchi nzima ikiongezeka kutoka takribani 1,200 mwaka 2000 hadi karibu 2,800 mwaka 2020, ishara ya kukua kwa Uislamu, licha ya shinikizo la kisiasa.

Kwa mujibu wa RNS News, katika vyuo vikuu mbalimbali, maimamu 80 wa muda wote sasa wanahudumu wakitoa huduma za kielimu, da'awah na msaada wa kiroho kwa wanafunzi Waislamu.

Rutgers University, kwa mfano, ina takribani wanafunzi 6,000 Waislamu na imekuwa na kituo maalumu cha maisha ya Kiislamu kinachowapa wanafunzi nafasi ya kuswali, kujifunza na kujenga jamii. Hii inaonyesha kuwa kizazi kilichokulia baada ya 9/11 hakijachagua kujificha, bali kujenga nafasi yake ndani ya jamii.

Pamoja na hayo, changamoto bado ni kubwa. CAIR ilipokea malalamiko 8,683 ya ubaguzi dhidi ya Waislamu mwaka 2025, idadi kubwa zaidi katika historia ya ripoti zake, huku malalamiko 198 yakihusishwa na uhalifu wa chuki.

Kwa mtazamo wa kisiasa, jambo la kutafakari ni kwa nini hofu dhidi yao huibuka kwa nguvu zaidi wakati wa uchaguzi. Kama huko nyuma, uchambuzi unaonyesha kuwa Uislamu unaatumiwa kama silaha ya kisiasa katika kampeni za 2026, huku wanasiasa kadhaa wakilenga wagombea Waislamu.

Lakini baada ya robo karne, historia inaonyesha picha tofauti: Waislamu wa Marekani hawajaondoka, wamejenga, wamejiandikisha kupiga kura, wamechaguliwa na wanaendelea kudai nafasi yao katika Marekani.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
0789 201383

# Kama Taifa, tusiruhusu dawa hizi zitudhuru

Wiki iliyopita, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilikamata mabegi 20 yaliyokuwa na dawa na vifaa tiba duni na visivyosajiliwa, vyenye thamani ya Sh310 milioni katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam.

Shehena hiyo iliyotokea nchini India ilinaswa baada ya wakaguzi wa TMDA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na maofisa wa forodha kubaini kuwa dawa hizo hazikuwa na usajili wala kibali cha kuingizwa nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dkt. Adam Fimbo, alisema ukubwa wa shehena hiyo umeibua wasiwasi, hasa ikizingatiwa kuwa miongoni mwa bidhaa zilizokamatwa ni dawa zinazotumika kutibu saratani, kifafa, shinikizo la damu na kisukari, pamoja na dawa aina ya Ozempic (semaglutide), inayotumika pia katika udhibiti wa uzito.

TMDA pia ilikamata shehena nyingine ya vifaa vya meno bandia pamoja na dawa za sindano, vyenye thamani ya takriban Sh50 milioni. Shehena hiyo ilijumuisha dawa za lignocaine, bupivacaine, adrenaline na vitamini.

Dkt. Fimbo alionya kuwa matumizi ya dawa zisizothibitishwa yanaweza kusababisha kuchelewa kupona, madhara makubwa kiafya, usugu wa dawa, ulemavu na hata kifo. Alisema hatari hiyo ni kubwa zaidi kwa wagonjwa wenye magonjwa sugu na makubwa, ikiwamo saratani, ambao maisha yao hutegemea ufanisi wa dawa wanazopewa.

Tunapata shida kuelewa kwa nini baadhi ya wafanyabiashara wanaingiza nchini dawa na vifaa tiba visivyokidhi viwango, huku wakitambua wazi kwamba hatua hiyo inaweza kuhatarisha afya na maisha ya wananchi.

Dawa si bidhaa ya kawaida. Mtu anayenunua dawa huwa anaweka afya na maisha yake mikononi mwa anayeiuza. Ndiyo maana biashara ya dawa za binadamu inapaswa kuendeshwa kwa uadilifu, uaminifu na uwajibikaji mkubwa, kwa kuwa kosa au uzembe katika biashara hiyo unaweza kugharimu maisha ya watu.

## Uislamu na fani ya tiba

Katika Uislamu, kulinda maisha ya mwanadamu ni jambo lililopewa uzito mkubwa. Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Haifai kujidhuru wala kumdhuru mwingine.” [Ibn Majah].

Hadith hii inasisitiza wajibu wa kila mmoja kuepuka vitendo vinavyoweza kusababisha madhara kwake au kwa wengine. Aidha, Uislamu unakataza ulaji wa mali kwa njia isiyo ya haki na unasisitiza uadilifu katika biashara.

Hivyo, mfanyabiashara anayefahamu kuwa bidhaa yake ni duni au haijathibitishwa, lakini akaamua kuiingiza sokoni kwa lengo la kujipatia faida, anapaswa kutafakari madhara ya kitendo hicho kwa Mwenyezi Mungu na kwa jamii.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: “Mwenye kufanya ghushi si katika sisi.” [Muslim]. Ujumbe huu uwazindue wafanyabiashara wanaoingiza nchini dawa hatarishi na kuziwasilisha kwa wananchi kana kwamba ni salama.

Pamoja na hayo, ni lazima tukiri kwamba wananchi wengi hawana uwezo wa kutambua dawa ambazo hazikidhi vigezo vya ubora na usalama. Hivyo, tunatoa rai kwa mamlaka husika kuendelea kuimarisha ukaguzi katika mipaka, viwanja vya ndege, bandari na masoko ili kuzuia uingizaji na usambazaji wa dawa zisizokidhi viwango.

Wafanyabiashara nao wanapaswa kutanguliza usalama wa wananchi badala ya kuweka mbele maslahi yao binafsi. Wakati Serikali ikiendelea kuboresha huduma za afya, juhudi hizo haziwezi kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwa dawa hatarishi zitaendelea kuingizwa na kusambazwa nchini.

Kama Taifa, tunapaswa kuwa na msimamo mmoja: Tusiruhusu dawa hizi zitudhuru. Afya na maisha ya wananchi lazima vipewe kipaumbele kuliko tamaa ya faida katika biashara.

SEHEMU YA MWISHO
2



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Uaminifu, msingi wa jamii bora na maadili mema



**Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulieleza aina mbalimbali za uaminifu katika Uislamu na namna unavyoweza kumjenga mtu binafsi na kuimarisha jamii kwa ujumla. Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, tunaendelea kuangazia aina nyingine za uaminifu na umuhimu wake katika maisha ya Muislamu.**

# Uaminifu, msingi wa jamii bora na maadili mema

## Uaminifu katika mazungumzo na uchaguzi wa viongozi

Muislamu anatakiwa kuwa mwangalifu katika maneno yake, kwa sababu neno linaweza kujenga au kubomoa, kuleta amani au kuchochea migogoro. Ukweli, uwazi na kuepuka uongo ni miongoni mwa misingi ya maadili ya Kiislamu.

Allah anasema: "Je, huoni vipi Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri, mizizi yake ni imara na matawi yake yanafika mbinguni..." [Qur'an, 14:24-26]. Aya hii inatukumbusha kuwa maneno mema huacha athari chanya, huku maneno mabaya yakivunja uhusiano na kuleta madhara kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

Uaminifu pia unahusisha namna tunavyowachagua watu wa kutuongoza au kutuwakilisha katika nafasi mbalimbali. Kiongozi ni mtu anayekabidhiwa dhamana ya kulinda maslahi ya wengine, kusimamia haki na kuhakikisha usalama na ustawi wa jamii.

Kwa msingi huo, si sahihi kumchagua mtu kwa sababu tu ni rafiki, ndugu au mtu wa karibu, wakati unajua hana uwezo wala uadilifu unaohitajika. Uongozi unapaswa kukabidhiwa kwa mtu mwenye uwezo, uelewa, uadilifu na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Madaraka yanapokosa uaminifu, yanaweza kutumiwa vibaya na kuleta madhara kwa jamii. Vivyo hivyo, uaminifu pekee bila uwezo unaweza kumfanya kiongozi ashindwe kutekeleza majukumu na wajibu aliopewa kwa ufanisi.

Mtume (rehema na amani za Allah zimshukie) alimwambia Abu Dharr (Allah amridhie) kuwa uongozi ni amana kubwa, na kwamba anayeshindwa kuibeba ipasavyo atakumbana na majuto Siku ya Kiyama

Kwa hiyo, uongozi haupaswi kuchukuliwa kama fursa ya kujinufaisha, bali ni dhamana nzito inayohitaji uwezo, uadilifu na uchamungu.

## Uaminifu katika mwili na nafsi

Mwili ni amana kutoka kwa Allah, hivyo unatakiwa kutunzwa na kulindwa dhidi ya mambo yanayoweza kuuharibu. Allah anasema: "Hakika masikio na macho na moyo; vyote hivyo vitaulizwa (Siku ya Kiyama)." [Qur'an, 17:36].

Muislamu anatakiwa kuepuka mambo yote yanayoweza kusababisha madhara, kujenga utamaduni wa kutunza afya na kufanya mazoezi kwa lengo la kuimarisha mwili na uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

Nafsi, pia ni amana inayopaswa kutunzwa na kulelewa katika mazingira yanayomsaidia mtu kumkumbuka Allah, kudumisha ibada, kutafakari na kujenga subira ya kukabiliana na changamoto za maisha bila kupoteza mwelekeo wala matumaini.

Aidha, ni muhimu kukabiliana na maumivu, msongo wa mawazo na changamoto za maisha kwa njia sahihi, badala ya kuruhusu hali hizo kumfanya mtu ajidhuru au kuwadhuru wengine.

## Uaminifu katika nasaha na biashara

Mtu anapokuomba ushauri, huwa amekukabidhi sehemu ya maisha yake na kukuonyesha imani aliyonayo kwako. Kwa hiyo, ushauri huo haupaswi kuchukuliwa kwa mzaha, kutumiwa kwa usaliti au kwa maslahi binafsi.

Anayepewa nafasi ya kutoa nasaha anapaswa kutumia uwezo na uelewa wake kumwelekeza mwenzake katika lililo bora, huku akihifadhi siri na heshima yake.

Biashara nayo ni eneo muhimu la kuonesha uaminifu. Mfanyabiashara anatakiwa kuwa mkweli kuhusu bidhaa, bei, vipimo na ubora wa anachouza.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Mfanyabiashara mkweli na mwaminifu atakuwa pamoja na Manabii, wakweli na mashahidi." Hii inaonesha kuwa biashara katika Uislamu si njia ya kutafuta kipato pekee, bali pia ni uwanja wa ibada na kujenga tabia njema.

## Uaminifu kwa watoto

Watoto ni miongoni mwa amana kubwa wanazokabidhiwa wazazi. Mtume amesema: "Kila mmoja wenu ni mchunga na ataulizwa kuhusu alichokichunga." Kwa hiyo, wajibu wa wazazi hauishii tu katika kuwapatia watoto chakula, mavazi na elimu ya kawaida.

Wanapaswa pia kuwajenga katika misingi ya imani na ibada, pamoja na kuwafundisha maadili, heshima na uwajibikaji. Mtoto anayelelewa kwa misingi hiyo hukua akiwa mtu mwenye uwezo wa kujitegemea, kulitumikia taifa na kutoa mchango chanya katika jamii.


## Njia za kukuza uaminifu

Uaminifu haujengwi kwa maneno pekee; unahitaji elimu, malezi na vitendo. Muislamu anapaswa kutambua kuwa uaminifu ni sehemu ya imani, na kwamba kudhoofika kwa uaminifu ni dalili ya udhaifu wa maadili na imani.

Njia nyingine ya kukuza uaminifu ni kuwa mfano bora kwa vitendo. Mtu anapokuwa mwaminifu katika maneno na matendo yake, huwavutia wengine kufuata mfano huo na hivyo kuchangia kujenga jamii yenye misingi imara ya uaminifu.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Tekeleza uaminifu kwa aliyekuamini, wala usimsaliti aliyekusaliti." Maana yake ni kwamba Muislamu hatakiwi kujibu hiyana kwa hiyana. Hata anapodhulumiwa, anatakiwa kusimama upande wa haki na uadilifu.

Uaminifu ukilindwa, hujenga imani, haki na uhusiano mwema; lakini ukipotea, huzaa usaliti, migogoro na uharibifu.



VISION 2050

ربيع ثان

NASAHA ZA WIKI
0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Muislamu, tubia haraka kabla mlango wa toba haujafungwa

Kuridhiwa na Allah ni miongoni mwa tunu kuu ambazo Muislamu anatamani kuzifikia, hasa katika Siku ya Kiyama. Ni taji la imani ya kweli, ibada, matendo mema, toba na maisha yanayolenga kumpendeza Muumba.

Mtu anapoteleza na kufanya makosa, hapaswi kukata tamaa wala kudhani kuwa hawezi tena kusamehewa. Badala yake, anapaswa kurejea kwa Mola wake, kutubu kwa dhati na kuchukua hatua za kurekebisha mwenendo wake.

Dhambi haipaswi kuwa sababu ya mtu kuwa mbali na Allah; badala yake inapaswa kuwa kichocheo cha kumkaribia zaidi kwa unyenyekevu, majuto na toba ya kweli. Qur'an yatwambia: "Hakika Allah anawapenda wanaotubu na anawapenda wanaojitakasa." [Qur'an, 2:222].

Aya hii inafungua mlango wa matumaini, lakini pia inatufundisha kuwa mtu hapaswi kufunga mlango wa toba kwa sababu ya makosa aliyowahi kufanya. Allah ametoa fursa kwa mwenye kukosea kujitathmini, kujutia makosa yake na kurejea kwake kupitia toba.

Tatizo hujitokeza pale mtu anapotenda dhambi na kuamua kuahirisha toba kana kwamba amepewa uhakika wa kuiona kesho. Baadhi husema watatubu baada ya kumaliza starehe zao au watakapofikia uzee.

Kwa sababu hiyo, wanaendelea kufanya madhambi wakijipa matumaini kwamba, siku moja watakapokuwa wazee watapata nafasi ya kutubu.

## Toba ina ukomo

Katika Sura ya An–Nisa (Qur'an, 4:18), Allah Mtukufu anasema: "Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti, kisha hapo akasema: Hakika sasa nimetubia. Wala wale wanaokufa hali ya kuwa ni makafiri. Hao tumewaandalia adhabu chungu."

Naye Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hakika Allah Aliyetukuka hukubali toba ya mja maadamu roho haijafika kooni." [Tirmidhi, Ahmad na Ibn Majah]. Kwa hiyo, epuka kauli "Nitatubu baadaye," kwa sababu muda wa kutubu una ukomo.

Ikiwa umeacha ibada, anza leo. Ikiwa umetumbukia katika madhambi, acha sasa. Ikiwa umemdhulumu mtu, mrejeshee haki yake. Usisubiri kesho, kwa sababu kesho ni ahadi ambayo mwanadamu hajapewa.

Kwa mchamungu, nasaha hizi ziwe chachu ya kuharakisha toba na kurekebisha mwenendo wake. Hii ni kwa sababu, kifo hakisubiri mtu atimize ndoto zake. Hivyo, tubu sasa kabla mlango wa toba haujafungwa.





Ni kujidanganya kudhani kuwa kwa sababu Allah ni Mwingi wa rehema, mtu anaweza kuendelea kufanya dhambi akitegemea kwamba atatubu wakati wowote atakapotaka. Huo ni mtego wa shetani, ambaye mara nyingi humfanya mwanadamu kuahirisha toba huku akiendelea kuzama katika dhambi.

Rehema ya Allah haipaswi kuwa kisingizio cha mja kuendelea kutenda dhambi, bali iwe sababu ya kuikimbilia toba kabla muda haujamwacha.

## Toba ni wajibu kwa kila kosa

Toba si jambo la hiari wala si ishara ya kushindwa au udhaifu. Ni mwanzo wa kujenga upya maisha, kurejesha uaminifu kwa Allah na wanadamu wenzetu, na hatimaye kurejea katika njia iliyonyooka.

Toba ya kweli si ile inayotamkwa kwa mdomo pekee. Ni mabadiliko yanayoanzia moyoni na kudhihirika katika tabia na matendo ya kila siku. Mja anapotambua kuwa amefanya kosa, anatakiwa kuliacha, kujutia kwa dhati alichokifanya na kuweka azma ya kutolirudia.

Mwenye busara ni yule anayeishi kati ya hofu na matumaini; anayehofia madhara ya dhambi, na anayatumainia rehema ya Allah na kutubu mara kwa mara anapokosea.

Busara yake huonekana katika utayari wa kutambua kosa, kulijutia, kulirekebisha na hatimaye kurejea katika njia iliyonyooka. Anatambua kuwa hakuna mwanadamu mkamilifu na kwamba kukosea ni sehemu ya udhaifu wa kibinadamu.

Allah anatwambia: "Enyi mlioamini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba ya kweli." [Qur'an, 66:8]. Aya hii inatukumbusha kuwa mlango wa toba uko wazi kwa kila anayechagua kutambua kosa lake, kutubu kwa dhati na kubadilika.

Jamii yenye watu wanaotambua makosa yao, wanaotubu na kusamehe ina nafasi kubwa ya kujenga amani, mshikamano na kuheshimiana.

Kwa hiyo, tunapokosea, tusikimbie ukweli wala kujificha nyuma ya visingizio. Tukubali makosa yetu, tuombe msamaha, turekebishe tulichoharibu na tubadilike.



SHEIKH Shaaban Mussa
0786 272 323

# ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

# Kuosha maiti: heshima ya mwisho ambayo Uislamu umempa Muislamu

**SEHEMU YA 5**

**Miongoni mwa mambo yanayoonesha ukamilifu wa Uislamu ni kwamba haukumheshimu Muislamu akiwa hai tu, bali umeendelea kumheshimu hata baada ya kufariki kwake. Moja ya heshima hizo ni kumuosha kwa utaratibu maalumu kabla ya kuswaliwa na kuzikwa.**

**Kwa bahati mbaya, baadhi ya watu huona kuosha maiti kuwa ni desturi ya kijamii au kazi ya watu maalumu. Ukweli ni kwamba kuosha maiti ni ibada yenye hukumu, masharti na adabu zake, kama zilivyo ibada nyingine.**

## Hukumu ya kuosha maiti

Wanazuoni wamekubaliana kwamba kumuosha Muislamu aliyefariki ni Faradhi Kifayah. Endapo baadhi ya Waislamu watatekeleza wajibu huu, wengine huondokewa na dhambi. Lakini ikiwa hakuna atakayemuosha bila sababu ya Kisharia, jamii yote inayoweza kutekeleza wajibu huo hubeba dhambi.

Hata hivyo, kuna baadhi ya maiti ambao Sharia imeweka hukumu tofauti, kama vile shahidi aliyekufa vitani kwa ajili ya dini. Hawa tutawazungumzia katika makala maalumu baadaye.

## Hekima ya kuosha maiti

Kuosha maiti si kwa sababu marehemu anahitaji usafi kama mtu aliye hai, bali ni sehemu ya kumheshimu na kumwandaa kwa safari yake ya mwisho duniani.

Ni maandalizi ya kukutana na Allah kwa heshima na utaratibu ambao Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametufundisha.

Kwa hiyo, anayemuosha maiti anapaswa kutambua kuwa anatekeleza ibada, si kazi ya kawaida.

## Dalili kutoka sunna

Dalili mashuhuri ni hadith ya Ummu 'Atwiyyah (Allah amridhie), alipofariki binti wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliwaambia wanawake waliokuwa wanamuosha: "Mwosheni mara tatu, au tano, au zaidi ya hapo mkiona inafaa; kwa maji na mkunazi, na katika mara ya mwisho wekeni kafuri, au kiasi cha kafuri..." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii ndiyo msingi wa fiqhi ya kuosha maiti, na ndani yake wanazuoni wamechambua hukumu nyingi kuhusu namna ya kuosha, idadi ya kuosha, na vitu vinavyopendekezwa kutumika.

## Nani anafaa kumwosha maiti?

Kanuni ya msingi ni kwamba anayemuosha maiti awe, kwanza, Muislamu; pili, mwenye uaminifu; tatu, mwenye kujua taratibu za kuosh na nne na mwisho, mwenye uwezo wa kuhifadhi siri za marehemu.

Hivyo, kimisngi, si kila anayejua kumwaga maji ndiye anayefaa kuosha maiti. Mwenye kuosha anatakiwa awe mtu mwenye taqwa, mpole na anayeheshimu utu wa marehemu.

## Je, Mume anaweza kumwosha mke wake? na mke kumwosha mume wake?

Hili ni miongoni mwa maswali yanayoulizwa sana, na jibu kwa hakika ni ndiyo.

Imepokewa kuwa Abubakr As-Swiddiq (Allah amridhie) alioshwa na mke wake Asmaa bint 'Umays (Allah amridhie). Kadhalika, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alimwambia Mama Aisha (Allah amridhie): "Lau ungefariki kabla yangu, ningekuosha na kukuvika sanda."

Hadith hii imepokewa na Imam Ahmad, Ibn Majah na wengine, na wanazuoni wengi wameitumia kuthibitisha kuwa mmoja wa wanandoa anaruhusiwa kumuosha mwenzake. Hivyo, ndoa inaendelea kutoa ruhusa hiyo hata baada ya mmoja wao kufariki.

## Adabu za mwenye kuosha

Anayemuosha maiti anatakiwa: kwanza, awe na nia ya kutafuta radhi za Allah, pili, ahifadhi heshima ya marehemu, tatu, asifunue sehemu za siri isipokuwa kwa kiwango cha lazima katika kuosha na asisimulie watu alichokiona katika mwili wa marehemu.

Imepokewa katika hadith kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwenye kumuosha Muislamu akaficha aliyoona kwake, Allah atamsamehe mara arobaini."

Ingawa wanazuoni wametofautiana kuhusu nguvu ya riwaya hii, maana yake imekubaliwa na wengi katika kuhimiza kuhifadhi siri na heshima ya maiti.

## Makosa yanayoonekana katika jamii

Baadhi ya makosa yanayotokea ni mara nyingi kwenye jamii ni kumruhusu kila mtu aingie mahali maiti anaoshwa, kupiga picha au kurekodi video wakati wa kuosha maiti na waoshaji kusimulia kasoro walizoziona kwenye mwili wa marehemu.

Makosa mengine yanayojitokeza mara nyingi ni kugeuza sehemu ya kuoshea maiti kuwa mahali pa mazungumzo na mzaha na kumuosha maiti kwa pupa bila kufuata utaratibu wa Sunna.

Hakika, vitendo hivi vinapingana na heshima ambayo Uislamu umeamrisha itolewe kwa marehemu.

## Tunajifunza nini?

Kuosha maiti si kazi ya mikono pekee, bali ni ibada ya moyo pia. Anayemuosha maiti anapaswa kutambua kwamba leo anamhudumia ndugu yake; kesho huenda yeye ndiye atakayehitaji kuhudumiwa na wengine. Kwa hiyo, afanye kazi hiyo kwa uaminifu, heshima na kwa kufuata Sunna.

Na Zaharani Baraka
018 424 258

# Usipuuze dhikri, huenda ikawa hazina yako Peponi

**Abu Musa al–Ash'ari (Allah amridhie) amesimulia kwamba, walipokuwa safarini pamoja na Mtume (rehema na amani zimshukie) kuelekea Khaybar, walipoingia kwenye bonde, watu waliinua sauti zao wakisema: "Allahu Akbar, Allahu Akbar, Laa ilaaha illa Allah." Mtume (rehema na amani zimshukie) akawaambia: "Enyi watu, zihurumieni nafsi zenu (punguzieni sauti), kwani hamumwombi kiziwi wala aliye mbali. Hakika Yeye anasikia yote na yuko pamoja nanyi." Abu Musa, ambaye alikuwa nyuma ya kipando cha Mtume akasema: "Laa hawla walaa quwwata illa billah." Mtume akamwambia: "Ewe Abdullah bin Qais! Je, nikufahamishe neno ambalo ni miongoni mwa hazina za Peponi?" Abu Musa akajibu: "Ndiyo, ewe Mtume wa Allah! Baba yangu na mama yangu wawe fidia kwako." Mtume akamwambia: "Laa hawla walaa quwwata illa billah." Kwa maana rahisi, kauli hiyo inamaanisha: "Hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Allah." [Bukhari].**

## Mafundisho ya tukio

Tukio hili linatufundisha umuhimu wa dhikri katika maisha ya kila siku. Kumtaja Allah mara kwa mara huleta utulivu wa moyo, humkaribisha mja zaidi kwa Mola wake na humsaidia kujiepusha na vishawishi vya shetani.

Moyo unapomkumbuka Allah hupata utulivu na faraja, lakini unapompuuza huathirika na hatimaye kupoteza mwelekeo wa lengo la kweli la maisha. Muislamu anapaswa kuuzoesha ulimi wake kumtaja Allah katika nyakati mbalimbali, iwe katika furaha, huzuni, shida au wakati wa utulivu.

## Namna ya kumtaja Allah

Abu Musa Al–Ash'ari (Allah amridhie) anatueleza kuwa watu walipofika katika bonde waliinua sauti zao kwa takbiri na tahlili. Mtume (rehema na amani zimshukie) akawaelekeza wapunguze sauti zao, akiwakumbusha kwamba Allah si kiziwi wala hayuko mbali nao.

Hii inaonesha kuwa Allah anasikia kila kitu; anajua maneno yanayotamkwa kwa sauti na yale yaliyofichika moyoni. Yeye yuko karibu na waja wake kwa elimu na ujuzi wake unaozunguka kila kitu.

Kwa msingi huo, ni vyema kupunguza sauti wakati wa kufanya dhikri, hasa pale ambapo hakuna sababu ya kuipandisha. Jambo hili halipingani na kupandisha sauti katika Talbiyah wakati wa ibada ya Hijja, kwa kuwa Talbiyah ni miongoni mwa alama za Hijja na inapaswa kudhihirishwa na kusikika.

Kwa ujumla, dhikri nyingine zinafaa kufanywa kwa sauti ya wastani, isipokuwa pale ambapo kuna sababu maalumu inayohitaji sauti ya juu.

## Maana ya "Laa hawla walaa quwwata illa billah"

Kauli ya "Laa hawla walaa quwwata illa billah" inamaanisha kwamba hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa msaada wa Allah.

Kauli hii humfundisha mwanadamu kutambua kwamba hawezi kujitegemea kikamilifu katika kila jambo. Hawezi kubadili hali, kujikinga na shari au kupata kheri kwa uwezo wake mwenyewe bila msaada, uwezo na matakwa ya Allah.

Wanazuoni wameifafanua kauli hiyo kwa mitazamo mbalimbali, wakieleza kuwa mwanadamu hana uwezo wa kujiepusha na maasi isipokuwa kwa ulinzi na hifadhi ya Allah, wala hana nguvu ya kudumu katika utiifu isipokuwa kwa msaada na taufiki yake.

Kwa mantiki hiyo, "Laa hawla walaa quwwata illa billah" ni tamko la kujisalimisha kwa Allah, kumtegemea na kutambua kuwa uwezo wote uko mikononi mwake.

## Hazina za Peponi

Mtume (rehema na amani zimshukie) alipomwambia Abu Musa kwamba "Laa hawla walaa quwwata illa billah" ni miongoni mwa hazina za Peponi, alisisitiza thamani na umuhimu mkubwa wa kauli hiyo.

Kauli hiyo inabeba mafunzo muhimu kuhusu kumtegemea Allah, kukiri udhaifu wa mwanadamu na kutambua kuwa mafanikio hayawezi kupatikana kwa uwezo wa binadamu pekee. Kwa kuwa hazina za Peponi ni nyingi, Muislamu anapaswa kuzitafuta kwa bidii kupitia utiifu, juhudi na matendo mema.

"Laa hawla walaa quwwata illa billah" si maneno ya kutamkwa kwa ulimi pekee, bali ni fundisho linalomwelekeza mja kumtegemea Allah, huku akiendelea kufanya juhudi na kutambua kuwa mafanikio ya kweli yanatokana na Allah.


Na Said Rajab
0783 650 803

# Maisha na urithi wa Mtume Muhammad

## SEHEMU YA MWISHO 2

**Katika makala iliyopita, tuliona namna Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie) alivyoweka misingi ya kuenea kwa Uislamu na kujenga jamii mpya iliyokuwa ikikua kwa kasi. Miongoni mwa misingi hiyo ilikuwa maandalizi ya msafara wa kijeshi kuelekea maeneo yaliyokuwa chini ya Himaya ya Warumi. Katika maandalizi hayo, Mtume alisisitiza pia misingi ya maadili ambayo yangepaswa kuzingatiwa na majeshi ya Waislamu – misingi ambayo baadaye ingekuwa sehemu muhimu ya mwongozo wa vita na uongozi katika historia ya Uislamu.**

**Leo tunahitimisha makala haya kwa kuangazia kwa upana zaidi maisha, misheni na urithi wa Mtume Muhammad (rehema na amani zimshukie).**



Urithi wa Mtume haukuishia katika masuala ya kijeshi wala upanuzi wa maeneo. Katika kipindi cha miaka 23 ya Utume, aliweka misingi ya mfumo mpana wa maisha uliogusa karibu kila nyanja ya jamii – kuanzia siasa na uongozi, uchumi na uhusiano wa kijamii, hadi ibada, maadili na mwenendo wa maisha ya kila siku.

Kwa maana hiyo, ujumbe wake haukuwa wa kujenga dola pekee, bali pia wa kumjenga mwanadamu na jamii inayosimama juu ya misingi ya imani, haki na uwajibikaji.

### Kukamilika kwa misheni ya Utume

Jukumu kuu la Mtume (rehema na amani zimshukie) lilikuwa kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kuwa mfano wa kuigwa kwa wanadamu. Baada ya miaka 23 ya Utume, jukumu hilo lilifikia tamati.

Qur'an Tukufu ilikuwa imefunuliwa, ikaandikwa katika nyenzo mbalimbali na, muhimu zaidi, kuhifadhiwa katika vifua vya Masahaba wengi. Utamaduni wa Waarabu wa wakati huo wa kuhifadhi na kukariri mashairi marefu ulikuwa miongoni mwa sababu zilizosaidia kuhakikisha Qur'an inahifadhiwa kwa njia ya kukariri.

Aidha, kauli, matendo na mwenendo wa Mtume vilihifadhiwa na kusambazwa miongoni mwa Masahaba na jamii za Waislamu katika maeneo mbalimbali ya Arabuni.

Miongoni mwa aya zilizofunuliwa katika kipindi cha mwisho cha uhai wake ni maneno ya Mwenyezi Mungu: "Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimeridhia Uislamu uwe Dini yenu..." [Qur'an, 5:3]. Aya hii inachukuliwa kuwa ishara muhimu ya kukamilika kwa Dini ya Uislamu.

### Kifo cha Mtume na kipindi cha mpito

Mwanzoni mwa kipindi cha kiangazi cha mwaka 632 BK, Mtume (rehema na amani zimshukie) alianza kuugua. Alisumbuliwa na maumivu makali ya kichwa na homa, hali iliyozidi kudhoofisha afya yake.

Kadiri ugonjwa ulivyoendelea, alihitaji msaada wa ndugu zake, akiwamo binamu yake Ali bin Abi Twalib na baba yake mdogo, Abbas (Allah awaridhie) ili aweze kutembea. Kwa sababu ya hali yake ya kiafya na kutoweza kuongoza sala za faradhi, alimteua Sahaba wake wa karibu na mwaminifu, Abubakr (Allah amridhie) kuwaongoza Waislamu katika sala.

Katika siku za mwisho za maisha yake, Mtume alikaa katika nyumba ya mkewe, Aisha bint Abubakr (Allah amuwie radhi). Katika kipindi hicho, jamii ya Waislamu iliendelea kutekeleza ibada na majukumu yake kwa kufuata mwongozo aliokuwa ameuweka.

### Urithi wa imani na umoja

Kifo cha Mtume kiliwatikisa sana Masahaba, ambao kwa miaka mingi walikuwa wameambatana naye katika safari nzito ya kuujenga Uislamu. Walishuhudia mateso na changamoto za mwanzo wa Uislamu huko Makka, wakapitia mapambano dhidi ya Makureish na hatimaye kushuhudia ushindi wa kuikomboa Makka.

Kwa miaka yote hiyo, Mtume alikuwa nguzo kuu ya mwongozo na uongozi wao, akiwaongoza katika masuala mbalimbali ya imani na maisha ya kila siku.

Kutajwa kwa kifo mara kwa mara na kutoweza kuongoza sala kulizidisha majonzi na wasiwasi miongoni mwa Masahaba. Mtume (rehema na amani zimshukie) alifariki mwaka 632 BK akiwa nyumbani kwa mkewe, Mama Aisha (Allah amuwie radhi).

Wakati huo, Waislamu walikuwa wamekusanyika, wengi wao wakitumaini kwamba angepata nafuu. Kifo chake kiliashiria mwisho wa enzi ya kwanza ya historia ya Uislamu – enzi iliyochukua miaka 23 ya Utume.

Na Said Rajab
0783 650 803

# Mchango wa Uislamu katika teknolojia ya AI

## SEHEMU YA MWISHO 4

**Katika sehemu iliyopita ya makala haya, tuliona jinsi Wanazuoni wa Kiislamu walivyochukulia maarifa kama amana yenye thamani kubwa, iliyopaswa kutumika kwa manufaa ya mwanadamu.**

**Wanazuoni hao pia walisisitiza umuhimu wa nia njema na uwajibikaji katika matumizi ya maarifa. Misingi hiyo bado ina uzito mkubwa katika dunia ya sasa, wakati ambapo mifumo ya Akili Unde inazidi kuwa na uwezo mkubwa na kutumika katika nyanja mbalimbali za maisha.**

**Katika sehemu hii ya pili na ya mwisho, tunaangazia mchango wa wanasayansi wa Kiislamu katika historia ya sayansi na teknolojia, na namna urithi huo unavyoweza kutusaidia kuelewa na kujenga mustakabali wa Akili Unde.**

**Wanasayansi wa Kiislamu wa Zama za Dhahabu za Uislamu walifanya kazi kwa unyenyekevu wa kifikra, huku wakitambua wazi mchango wa waliowatangulia, wakiwamo Wagiriki, Wahindi na Waajemi.**

**Mtazamo huo unatofautiana na baadhi ya simulizi za historia ya Ulaya, ambazo mara nyingi zimepuuza au kutotilia maanani mchango wa wanasayansi kutoka nje ya Ulimwengu wa Magharibi.**

**Kurejesha muktadha huu wa kihistoria kunatusaidia kujenga simulizi jumuishi na sahihi zaidi kuhusu maendeleo ya sayansi duniani.**

### Kwa nini jambo hili ni muhimu

Kupuuza mchango wa wanasayansi wa Kiislamu katika dhana na maarifa ya awali yaliyojenga msingi wa teknolojia ya Akili Unde kunaongeza hatari ya kupoteza sehemu muhimu ya kumbukumbu ya kihistoria.

Kupuuza historia hiyo kunaweza kufuta mchango wa watu na tamaduni kutoka nje ya Ulimwengu wa Magharibi katika maendeleo ya teknolojia hii muhimu. Pia kunaweza kupotosha uelewa wa historia ya sayansi na kudhoofisha fursa za ushirikiano wa kimataifa.

Kusahihisha rekodi hii kunasaidia kujenga historia jumuishi zaidi ya chimbuko na maendeleo ya teknolojia ya Akili Unde. Zaidi ya hapo, kunatoa fursa ya kuhamasisha vizazi vijavyo na kukuza uaminifu katika ubunifu na utafiti wa kisayansi katika taaluma mbalimbali.

Isitoshe, kuwatambua wanafikra hawa wa awali wa Kiislamu kunahimiza mbinu shirikishi zaidi za uvumbuzi.

Kama ambavyo al–Khwarizmi, al–Kindi, Ibn Sina na al–Jazari walijenga maarifa kwa kuunganisha tamaduni na mila mbalimbali, watafiti wa Akili Unde wa leo wanapaswa kuendelea kuunganisha mitazamo tofauti ili kukabiliana na changamoto tata za kimaadili zinazokabili teknolojia hii.

### Kurejesha uadilifu katika historia ya Akili Bunifu

Watu mashuhuri wa zama za Mwamko wa Ulaya, akiwamo Nicolaus Copernicus na Isaac Newton walijenga sehemu ya maarifa yao juu ya kazi za awali za Kiislamu na tamaduni nyingine zisizo za Ulaya.

Hata hivyo, mara nyingi michango na vyanzo hivyo havikutambuliwa ipasavyo katika simulizi za baadaye za historia ya sayansi.

Kwa mfano, kuna hoja za kihistoria kwamba Copernicus huenda alifaidika na dhana za unajimu zilizotengenezwa na Nasir al–Din al–ʿusi. Vivyo hivyo, tafiti za Ibn al–Haytham kuhusu mwanga na mfumo wa kuona zilitoa msingi muhimu kwa maendeleo ya baadaye ya fizikia ya mwanga (optics) kabla ya tafiti za Johannes Kepler.

Kutambua viungo hivi vya kihistoria kunasaidia kurejesha usawa katika simulizi ya maendeleo ya sayansi na kuimarisha ukweli kwamba sayansi ni safari ya pamoja ya wanadamu.

Mwelekeo huo hauishii katika ulimwengu wa Kiislamu pekee. Uvumbuzi wa kale kutoka China, kama vile utengenezaji wa karatasi na baruti uliathiri kwa kiasi kikubwa historia ya dunia. Hata hivyo, katika baadhi ya simulizi za Magharibi, michango hiyo imekuwa ikisimuliwa bila kutambua kikamilifu chimbuko lake na watu waliowezesha maendeleo hayo.

### Hitimisho


Zama za Dhahabu za Uislamu hazikuwa tu daraja kati ya sayansi ya kale na sayansi ya kisasa. Zilikuwa pia kipindi cha uvumbuzi mkubwa wa kisayansi na kiteknolojia, ambao uliathiri moja kwa moja maendeleo ya maarifa yanayohusishwa na teknolojia ya Akili Unde tunayoiona leo.

Kwa kuheshimu urithi wa al–Khwarizmi, al–Kindi, Ibn Sina na al–Jazari, tunapata fursa ya kusimulia historia ya maendeleo ya kisayansi kwa usahihi na kwa mtazamo jumuishi zaidi. Hii ni historia inayosisitiza ushirikiano, unyenyekevu wa kifikra na hekima ya pamoja iliyojengwa na tamaduni mbalimbali duniani.

Uelewa wao kuhusu mantiki, utambuzi, mifumo otomatiki na maadili unaendelea kuwa na umuhimu katika mjadala na utafiti wa teknolojia ya Akili Unde hadi leo.

Kadiri tunavyoelekea kwenye mifumo yenye uwezo mkubwa zaidi wa kiakili, ni muhimu kukumbuka kwamba misingi ya teknolojia ya Akili Unde haikujengwa na jamii moja wala katika kipindi kimoja.

Ilijengwa hatua kwa hatua kwa karne nyingi kupitia ubadilishanaji wa maarifa, mwingiliano wa tamaduni na michango ya wanafikra kutoka sehemu mbalimbali za dunia.



**John McCarthy baba wa akili bandia (Artificial Intelligence - AI). Yeye ndiye aliyebuni neno "Artificial Intelligence" na kuweka misingi ya tawi hili la sayansi mwaka 1956.**

SEHEMU YA 1

# Mnapotuandaa kwa harusi kuliko maisha ya ndoa ni tatizo

**Sisi vijana tunapoelekea kuoa au kuolewa, kuna mambo mawili ambayo wazazi wetu na jamii inapaswa kuyatenganisha vizuri: maandalizi ya harusi na maandalizi ya ndoa.**

**Maandalizi ya harusi yanahusu tukio. Tunapanga siku ya kufunga ndoa, ukumbi, chakula, mapambo, mavazi, usafiri, wapiga picha, wageni na matumizi mengine ya sherehe.Maandalizi ya ndoa, kwa upande mwingine, yanawahusu watu wawili ambao baada ya sherehe hiyo watatakiwa kuishi pamoja kama mume na mke.**

**Harusi inaweza kuchukua saa chache, imezidi siku chache, pengine wiki ya matukio tofauti. Ndoa tunatarajia idumu miaka mingi, ikiwezekana maisha yote.**

**Lakini ni wazi tunaweka kipaumbele cha maandalizi kwa tukio la saa chache kuliko lile la kuwaandaa watu kwa maisha yatakayopelekea uzazi na malezi.**

**Miezi kadhaa kabla ya harusi familia zinaweza kuwa na vikao vingi. Bajeti inapangwa. Michango inatafutwa. Ukumbi unatembelewa. Mavazi yanajadiliwa. Wageni wanahesabiwa. Tunajua watakula nini, watakaa wapi na nani atapiga picha. Lakini je, ni vikao vingapi vinavyofanyika kuwauliza wale wawili: Mnaelewa kweli maisha mnayokwenda kuanza? Hapo ndipo tunapokosea.**

**Harusi ni muhimu. Ni tukio la furaha, heshima na kutangaza muungano wa watu wawili mbele ya familia na jamii. Hakuna sababu ya kuidharau. Lakini harusi si ndoa.**

## Baada ya wageni kuondoka

Siku ya harusi itapita. Chakula kitaisha. Maua yatanyauka. Nguo maalumu zitawekwa kabatini. Picha zitabaki kwenye simu na albamu.

Kisha watu wawili watabaki wenyewe. Hapo hakuna tena kamati ya harusi.

Kutakuwa na nyumba ya kuendesha. Kuna fedha za kusimamia. Kuna mahusiano ya kimapenzi. Kuna ndugu wa pande mbili. Kuna tofauti za tabia. Kuna hasira. Kuna matarajio kuhusu watoto, kazi, majukumu ya nyumbani na namna ya kutumia fedha.

Mmoja anaweza kuamini mume anatakiwa kufanya jambo fulani; mwingine hajawahi hata kusikia matarajio hayo.

Mmoja anaingia na madeni ambayo mwenzake hakuyajua. Mwingine ana mtazamo tofauti kuhusu ndugu kuingilia mambo ya familia. Mmoja akikasirika hunyamaza; mwingine anataka tatizo lijadiliwe hapo hapo. Hayo ndiyo maisha ya ndoa.

Na hapa ndipo umuhimu wa maandalizi ya ndoa unapojitokeza.

Ukiwekeza muda, fedha na nguvu nyingi katika kupanga harusi lakini hukuwasaidia wanaooana kujifunza kuwasiliana, kutatua migogoro, kuendesha fedha na kuelewa majukumu yao, umepamba mlango lakini hujaimarisha nyumba.

Madhara yake yanaweza kuanza mapema. Watu wanaingia kwenye ndoa wakiwa na matarajio yasiyowahi kujadiliwa.

Tofauti ndogo zinakuwa migogoro mikubwa. Fedha zinakuwa chanzo cha ugomvi. Ndugu wanaingilia kwa sababu wenzi wenyewe hawana mfumo wa kutatua tofauti zao. Na wakati mwingine tunafanya jambo baya zaidi: tunaanza maisha mapya ya ndoa na deni la sherehe ya siku moja.

## Tujifunze kwa wengine

Katika baadhi ya dini nyingine Tanzania, maandalizi ya maisha ya ndoa kabla ya kufunga ndoa (kwa maana ya mafunzo) yamejengeka kama sehemu rasmi ya mchakato. Kwa upande wetu Waislamu Tanzania Bara, jitihada zipo lakini bado hatuna utaratibu au utamaduni ulioenea wa kuwapa vijana wanaotaka kuoa au kuolewa mafunzo ya kina ya kabla ya ndoa.

Kwa wengi, maandalizi yanabaki kwa kiasi kikubwa kwenye ushauri wa ndugu, makungwi na mawaidha yanayotolewa wakati ndoa tayari ipo mlangoni. Makungwi wanaweza kuwa na uzoefu na maarifa yenye manufaa. Tatizo ni kwamba hayana kiwango kimoja cha elimu. Si kila anayefundisha ana msingi wa kutosha wa dini, saikolojia ya mahusiano, afya, mawasiliano au usimamizi wa fedha.

Halafu tunategemea mawaidha ya siku ya ndoa. Sheikh anapata dakika kadhaa kumwambia mume haki za mke na kumwambia mke haki za mume. Wageni wanataka kula, wengine wanazungumza, watu wana haraka ya kuendelea na sherehe.

Tunatarajia dakika hizo zibebe elimu ambayo ilipaswa kutolewa kwa wiki kadhaa, kama sio miezi. Waswahili wanasema: mbuzi hanenepi mnadani.

## Zanzibar imeanza kutengeneza njia

Zanzibar angalau imepiga hatua katika eneo hili.

Ofisi ya Mufti Mkuu imekuwa ikiendesha mafunzo ya maadili ya ndoa kwa wananchi na wanandoa watarajiwa na niliwahi kusikia tathmini ilionesha kiwango cha talaka ni kidogo miongoni mwa waliopitia mafunzo hayo kuliko wasiopitia. Lakini hata bila utafiti, hawalingani na wasiojua. Hivyo basi, tunapaswa kuunda programu za kuwaandaa watu kwa maisha ya ndoa, hasa huku bara.

Tunaweza kuendelea kuwa na harusi nzuri, ndani ya mipaka ya Kiislamu lakini uzuri wa harusi usiwe mkubwa kuliko ubora wa maandalizi ya ndoa.

Wiki ijayo nitaendelea na sehemu ya pili: Ni mambo gani hasa mwanamume na mwanamke wanaotarajia kuoana wanapaswa kufundishwa kabla ya ndoa, kwa utafiti na mtazamo wangu.

Mwisho, Nisisitize hatuhitaji tu vijana wanaojua namna ya kuandaa harusi. Tunahitaji wanaume na wanawake walioandaliwa kuwa waume na wake.

ربيع ثان

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

# Maneno 9 epuka kuyatamka kazini

**Mahali pa kazi, uwezo pekee hautoshi. Unaweza kuwa mchapakazi, mwenye elimu nzuri na mwenye mawazo bora, lakini namna unavyowasiliana na wengine inaweza kujenga au kuharibu taswira yako kitaaluma.**

**Wakati mwingine tatizo si kile tunachomaanisha, bali namna tunavyokisema. Sentensi moja inaweza kukufanya uonekane mkorofi, hata kama hilo halikuwa kusudi lako. Haya ni maneno na kauli 10 unazopaswa kuzitumia kwa tahadhari kazini.**

### "Umekosea"

Kutofautiana kwa mawazo ni jambo la kawaida kazini. Tatizo huanza pale tunapofanya mjadala wa hoja kuwa mashindano ya nani yuko sahihi.

Kumwambia mwenzako moja kwa moja, "Umekosea," kunaweza kumweka katika hali ya kujitetea. Badala ya kujadili hoja, mjadala unaweza kugeuka kuwa mgongano wa watu.

Ni bora kusema: "Nina wazo jingine ambalo linaweza kutusaidia." Hujaficha msimamo wako, lakini umefungua mlango wa majadiliano.

### "Nilidhani mtu mwingine angefanya"

Hii ni mojawapo ya sentensi zinazoweza kuharibu taswira yako ya uwajibikaji. Inaonyesha kwamba jukumu halikufuatiliwa na sasa lawama zinahamishiwa kwa mtu mwingine.

Badala yake, kubali sehemu yako. Sema: "Nilipaswa kuthibitisha mapema nani alikuwa anawajibika." Uwajibikaji hujenga uaminifu kuliko kutafuta mtu wa kulaumiwa.

### "Siwezi kufanya kazi na mtu huyo"

Ofisini hutachagua kila wakati watu unaotaka kufanya nao kazi. Kutakuwa na tofauti za hulka, mitazamo na mbinu za kufanya kazi.

Ukisema huwezi kufanya kazi na mtu fulani, unaweza kuonekana kama mtu asiyeweza kuendana na mazingira tofauti.

Badala yake uliza: "Tunawezaje kuboresha namna tunavyoshirikiana?" Hapo unahamisha mjadala kutoka kwa mtu kwenda kwenye suluhisho.

### "Ulipaswa kufanya..."

"Ulipaswa kuniambia mapema." "Ulipaswa kujua." "Ulipaswa kuwasilisha jana."

Maneno haya mara nyingi huangalia kosa lililotokea kuliko namna ya kulizuia lisijirudie.

Kazini, hasa panapohitajika ushirikiano, lugha inayotafuta suluhisho huwa na tija zaidi.

Sema: "Wakati mwingine tafadhali nijulishe mapema," au "Tuhakikishe tunapanga hili mapema zaidi."

### "Tumekuwa tukifanya hivi siku zote"

Hii ndiyo sentensi maarufu ya kupinga mabadiliko. Inawezekana kabisa mfumo wa zamani unafanya kazi vizuri. Lakini kusema tu, "Tumekuwa tukifanya hivi siku zote," kunaweza kukufanya uonekane umefungwa na mazoea.

Badala yake uliza: "Njia hii mpya itatupa faida gani?" Hapo unatathmini mabadiliko badala ya kuyakataa bila kuyachunguza.

### "Labda nimekosea, lakini..." au "Huenda hili ni wazo la kijinga..."

Usiliue wazo lako kabla wengine hawajalisikia. Watu wengi hutumia sentensi hizi kujikinga dhidi ya kukosolewa. Lakini mara nyingi matokeo yake ni kudhoofisha ujumbe wao wenyewe.

Kama una hoja, iwasilishe kwa utulivu na kujiamini. Badala ya kusema, "Huenda hili ni wazo la kijinga," sema: "Ninapendekeza tujaribu njia hii." Wazo lako bado linaweza kupingwa, lakini angalau umelipa nafasi ya kusikilizwa.

### "Hii si haki"

Huenda kweli hali si ya haki. Labda umepewa kazi nyingi kuliko wengine, umepitwa kwenye nafasi ya kupandishwa cheo au unaona mgawanyo wa majukumu hauna uwiano.

Lakini kulalamika kwa kusema tu, "Hii si haki," hakuelezi tatizo wala suluhisho. Ni bora kuzungumza na msimamizi wako kwa ushahidi: eleza mzigo wa kazi, matarajio na kile unachoomba kibadilike. Tofautisha kati ya kulalamika na kuwasilisha hoja.

### "Hilo haliwezekani"

Kabla hujasema jambo haliwezekani, jiulize: Haliwezekani kabisa, au ni gumu tu? Waajiri wengi huthamini wafanyakazi wanaoweza kuona changamoto na bado wakatafuta njia.

Badala ya kufunga mjadala kwa kusema, "Haiwezekani," sema: "Hebu tuangalie njia zinazowezekana." Huenda jibu likabaki kuwa hapana, lakini litakuwa jibu lililofikiwa baada ya kuchunguza uwezekano.

### "Nitajaribu"

Kwa lugha ya kawaida, "nitajaribu" inaweza kuonekana kuwa kauli nzuri. Kazini, hata hivyo, inaweza kuacha sintofahamu: Utafanya au hutafanya?

Ikiwa unaona muda au rasilimali ni changamoto, eleza hilo moja kwa moja.

Sema: "Nitahitaji msaada kidogo ili kukamilisha ndani ya muda, lakini nitahakikisha kazi inafanyika."

Hiyo ni ahadi yenye uhalisia kuliko "nitajaribu."

### Maneno hujenga taswira yako

Mawasiliano ya kitaaluma hayamaanishi kujifanya au kuogopa kusema ukweli. Yanamaanisha kujua namna ya kusema ukweli bila kufunga milango ya ushirikiano.

Mara nyingi tofauti kati ya mfanyakazi anayeonekana mgumu na yule anayeonekana mkomavu si hoja wanayotoa. Ni namna wanavyoitoa.

Kabla hujasema jambo kazini, jiulize swali moja rahisi: Je, maneno yangu yanasaidia kutatua tatizo, au yanaongeza tatizo jingine?

Jibu la swali hilo linaweza kubadili kabisa namna watu wanavyokuona kazini.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

# Ujuzi aina 7 siri ya viongozi waliofanikiwa

**KATIKA mazingira ya sasa ya kazi, teknolojia inaweza kusaidia viongozi kuchambua taarifa, kupanga kazi, kuandika ripoti na hata kufanya baadhi ya maamuzi kwa haraka. Lakini bado kuna eneo ambalo mashine haiwezi kulichukua kirahisi: uwezo wa binadamu kuelewa watu, kujenga uaminifu, kuwasiliana kwa hisia na kuongoza wengine kupitia changamoto.**

**Hapo ndipo kile kinachoitwa soft skills—ujuzi wa kibinadamu na kijamii—kinapokuwa muhimu.**

**Kiongozi anaweza kuwa na elimu kubwa, uzoefu wa miaka mingi na uwezo wa kiufundi, lakini bila ujuzi wa kushughulika na watu, anaweza kushindwa kujenga timu inayomwamini na inayotaka kufanya kazi pamoja naye.**

**Hizi ni sifa saba zinazojitokeza kwa viongozi wanaofanikiwa.**

## Mosi, uhalisia na uaminifu

Kiongozi mwenye nguvu si yule anayejifanya hana dosari. Ni yule anayekuwa wa kweli, muwazi na mwenye msimamo unaoonekana katika maneno na matendo yake.

Watu wanapotambua kwamba kiongozi anasema anachomaanisha na kutenda anachosema, uaminifu huanza kujengwa.

Uhalisia pia unamaanisha kutokuwa na sura tofauti mbele ya watu tofauti. Kiongozi anapaswa kuwa na misingi inayotabirika. Wafanyakazi wasiwe wanajiuliza kila siku: "Leo tumempata katika hali gani?" Uthabiti katika tabia huleta usalama katika timu.

## Pili, uwezo wa kuelewa hisia za wengine

Kiongozi mzuri haharakishi kutoa jibu kila wakati. Anajifunza kwanza kusikiliza.

Kabla ya kutoa maoni yako, uliza swali moja zaidi. Mfanyakazi akisema ana changamoto, badala ya kuanza mara moja kumfundisha cha kufanya, unaweza kuuliza: "Ni sehemu gani hasa inakusumbua zaidi?"

Swali hilo dogo linaweza kufungua jambo kubwa.

Kuelewa hisia za wengine hakumaanishi kukubaliana nao kila wakati. Ni kujaribu kuona jambo kupitia macho yao kabla ya kutoa uamuzi. Mtu anapojisikia amesikilizwa, hata uamuzi usiompendeza unaweza kuwa rahisi kuupokea.

## Tatu, uwezo wa kuinuka baada ya changamoto

Uongozi hauna mafanikio pekee. Kuna mipango itakayoshindwa, wateja watakaoondoka, miradi itakayochelewa na maamuzi yatakayokuja na matokeo yasiyotarajiwa. Kiongozi anayefanikiwa anahitaji uwezo wa kusimama tena.

Haimaanishi kutoumizwa na kushindwa. Inamaanisha kutoruhusu kushindwa kwa jambo moja kuharibu uwezo wa kuendelea.

Badala ya kuuliza tu, "Nani amekosea?", kiongozi imara anauliza pia: "Tumejifunza nini na tutafanya nini tofauti safari ijayo?"

Timu hujifunza sana kutokana na namna kiongozi anavyoshughulikia siku mbaya.

## Nne, unyenyekevu

Cheo kinaweza kumshawishi mtu kuamini yeye ndiye mwenye majibu yote. Hapo ndipo matatizo huanza.

Kiongozi mwenye unyenyekevu anaweza kusema, "Sijui," au, "Wazo lako ni bora kuliko langu." Anatambua mafanikio ya watu wake na kuwapa sifa wanazostahili. Badala ya kusema tu "kazi nzuri", anataja jambo walilofanya vizuri na kwa nini lilikuwa na umuhimu.

Pia anatafuta maarifa kutoka kwa watu wenye uzoefu tofauti na wake. Utaalamu ni muhimu, lakini unyenyekevu humzuia kiongozi kugeuza uzoefu wake kuwa ukuta unaozuia mawazo mapya.

## Tano, uwajibikaji

Kiongozi anayetaka timu yake iwajibike lazima yeye mwenyewe awe wa kwanza kufanya hivyo. Akiamua vibaya, akubali. Akiahidi jambo, alifuatilie. Akikosea, asiwe na haraka ya kutafuta mtu wa kumbebesha lawama.

Sentensi rahisi kama, "Hili lilikuwa kosa langu, na nitalirekebisha," inaweza kujenga uaminifu zaidi kuliko maelezo marefu ya kujitetea.

Kulinda taswira yako kila wakati kunaweza kukupunguzia heshima. Kukubali kosa kwa wakati kunaweza kukuongezea.

## Sita, mawasiliano mazuri

Kiongozi hawezi kuongoza watu ambao hawaelewi anachotaka. Mawasiliano mazuri yanahitaji uwazi, kusikiliza na kutoa nafasi ya maswali. Lakini mawasiliano yasibaki kwenye maagizo na tarehe za kumaliza kazi pekee.

Ni muhimu pia kuwa na mazungumzo ya ana kwa ana na watu wa timu mara kwa mara. Muulize mfanyakazi anaendeleaje, anajifunza nini, ana changamoto gani na anataka kukua katika eneo gani.


Wakati mwingine taarifa muhimu zaidi kuhusu taasisi haipatikani kwenye ripoti. Inapatikana katika mazungumzo ya kawaida.

## Saba, mtazamo chanya wenye uhalisia

Kiongozi mwenye matumaini si yule anayejifanya kila kitu kiko sawa. Ni yule anayekubali changamoto lakini anasaidia timu kuona kwamba bado kuna njia ya kwenda mbele.

Tatizo likitokea, haongezi hofu isiyo ya lazima. Anaelekeza nguvu kwenye suluhisho, wakati maneno yake yanaweza kuwafanya watu waone ukuta au waone mlango.

Ndiyo maana matumaini ya kiongozi yanapaswa kwenda sambamba na uhalisia. Si kusema, "Hakuna tatizo." Ni kusema, "Tatizo lipo, lakini hebu tuangalie tunachoweza kufanya." Mwisho wa yote, ujuzi wa kiufundi unaweza kumsaidia



# Kupata 'A' muhimu lakini pia mfundishe mwanao haya 10

**MTOTO anaweza kufanya vizuri sana darasani, kupata alama za juu na kuonekana mwenye mafanikio, lakini bado akawa hajaandaliwa vya kutosha kukabiliana na maisha ya utu uzima.**

**Elimu ni muhimu. Alama nzuri zina nafasi yake. Lakini malezi hayaishii kwenye matokeo ya darasani.**

**Kuna mambo ambayo hayapimwi kwenye mtihani: kukubali kosa, kusema ukweli, kutimiza ahadi, kuvumilia matokeo ya maamuzi yako, kumaliza ulichoanza na kuwa na uwezo wa kujiongoza wakati hakuna mzazi anayekuangalia.**

**Kwa wazazi wanaolea wavulana, hasa wanaoingia ujana, haya ni mambo 10 muhimu ya kuwafundisha sambamba na elimu ya darasani.**

## Mosi, ajifunze kusema: "Nilikosea"

Kukiri kosa bila kutafuta sababu ya kujitetea ni ishara ya uwajibikaji. Mtoto asizoezwe kuamini kwamba lazima kila mara athibitishe kuwa yuko sahihi. Afundishwe kuwa kusema "nilikosea" hakumpunguzi thamani.

Kinachofuata baada ya kosa ndicho muhimu zaidi: atajifunza nini, na atafanya nini kulirekebisha?

## Pili, aseme ukweli hata unapomgharimu

Ni rahisi kusema ukweli unapokuwa hauna madhara. Jaribu la kweli linakuja pale kusema ukweli kunapoweza kusababisha adhabu, aibu au kupoteza kitu anachokipenda.

Mvulana anayejifunza kusema ukweli katika mazingira hayo anajengewa msingi wa uaminifu ambao atahitaji akiwa mwanafunzi, mfanyakazi, mume, baba au kiongozi.

## Tatu, atekeleze ahadi

Ahadi ndogo ndogo ndizo zinazojenga tabia. Kama amesema atasafisha chumba chake, amalize. Kama amepewa jukumu fulani nyumbani, asilifanye tu baada ya kukumbushwa mara tano.

Lengo si kumgeuza mtoto kuwa mashine ya kutii maagizo, bali kumfundisha kwamba neno lake lina thamani.

## Nne, akubali kuwajibika

Wazazi wakati mwingine, kwa upendo, hujaribu kuwaokoa watoto katika kila hali ngumu. Lakini mtoto akifanya kosa na kila mara mzazi akafuta matokeo yake, anaweza kuchelewa kujifunza uhusiano kati ya uamuzi na matokeo.

Matokeo yanapaswa kuwa ya kiasi na yanayoendana na kosa, lakini yawepo. Aelewe: ulichofanya kina matokeo, na si lazima kila mara mtu mwingine abebe gharama yake.

## Tano, asiishie kuomba msamaha tu — arekebishe alichoharibu

Kuomba msamaha ni muhimu, lakini wakati mwingine hakutoshi. Kama amevunja kitu, afikirie namna ya kukirekebisha. Kama amemuumiza mtu, ajifunze kwamba kurejesha uhusiano kunahitaji zaidi ya kusema "samahani."

Uwajibikaji ni pamoja na kurekebisha madhara kadiri inavyowezekana.

## Sita, amalize anachoanza

Maisha yana kazi nyingi zisizosisimua. Mtoto anayefundishwa kuacha kila kitu kinapokuwa kigumu anaweza kuingia utu uzima akiwa na tabia ya kuanza mambo mengi na kumaliza machache.

Kumfundisha kumaliza alichoanza humjengea uvumilivu, nidhamu na uwezo wa kutekeleza majukumu hata pale hamasa imepungua.

## Saba, ajifunze kudhibiti hisia asipopata anachotakA

Kukataliwa, kushindwa au kunyimwa jambo ni sehemu ya maisha. Mvulana anahitaji kujifunza kushughulikia hasira na kukatishwa tamaa bila matusi, fujo au kulipiza kisasi.

Haimaanishi asioneshe hisia. Maana yake ni kwamba ajifunze kuwa hisia zake ni halali, lakini hazimpi ruhusa ya kufanya kila anachotaka.

## Nane, aombe msaada anapouhitaji

Kujifanya "ninaweza kila kitu" si nguvu. Mvulana anayejifunza kuomba msaada anapokwama ana nafasi nzuri zaidi ya kujifunza na kurekebisha tatizo mapema.

Kumwomba mwalimu maelezo, kumwambia mzazi amechanganyikiwa au kukiri kuwa hawezi kutatua jambo fulani si udhaifu. Ni kujitambua.

## Tisa, ajue wakati wa kuondoka kwenye kundi

Moja ya mitihani mikubwa ya ujana ni shinikizo la marafiki. Afundishwe kwamba si kila jambo ambalo kundi linafanya lazima naye afanye.

Kuna nyakati atalazimika kuchagua kati ya kukubalika na watu na kusimamia anachojua ni sahihi.

Uwezo wa kusema, "Hili silifanyi," unaweza kumuepusha na maamuzi mengi yatakayokuja kumgharimu.

## Kumi, aelewe kuwa kuwajibika si udhaifu

Uwajibikaji si adhabu. Ni sehemu ya uongozi binafsi.

Mvulana anaposema, "Hili lilikuwa jukumu langu," anapoomba msamaha, kurekebisha kosa na kutimiza ahadi, anajifunza kujiongoza mwenyewe.

Na hapo ndipo malezi yanapolenga kufika. Kwa sababu mzazi hatakuwa pembeni ya mtoto milele akimwambia afanye nini.

Katika kipindi cha ujana, uwezo wa kupanga, kujidhibiti, kufanya maamuzi na kujifunza kutokana na matokeo bado unaendelea kukua. Ndiyo maana watoto wanahitaji nafasi za mara kwa mara za kufanya mazoezi ya uwajibikaji, si kusikiliza mihadhara kuhusu uwajibikaji pekee.

Wazazi wanaweza kuweka viwango vya juu huku wakiendelea kuwa chanzo cha upendo na usalama. Ujumbe uwe: "Unawajibika kwa ulichofanya. Lakini bado tunakupenda, na unaweza

Na Samrath Msuya
0789 201 383

# Ubunifu katika ufundishaji hisabati

**SEHEMU YA 2**

**Katika makala iliyopita tuliona kwamba changamoto ya hisabati haiwezi kuelezwa kwa kusema tu kwamba baadhi ya watoto "hawana kipaji" cha somo hilo. Namna tunavyowafundisha, tunavyowapa nafasi ya kujaribu na hata tunavyowachukulia wanapokosea inaweza kuathiri sana namna wanavyoiona hesabu. Sasa tujiulize swali jingine: Mwanafunzi anayepata jibu sahihi, je, ameelewa hesabu? Si lazima.**

Anaweza kuwa amekariri hatua alizooneshwa na mwalimu. Anaweza pia kuwa amefanya mazoezi ya aina hiyo mara nyingi kiasi kwamba anajua anachotakiwa kufanya bila kuelewa kwa kina kwa nini anafanya hivyo. Tatizo hujitokeza swali linapobadilishwa kidogo.

Hivyo, ufundishaji wa hesabu haupaswi kuishia kwenye kumfikisha mtoto kwenye jibu. Unapaswa pia kumjengea uwezo wa kufikiri, kuuliza, kujaribu na kueleza. "Umefikiaje jibu hilo?" Hili linaweza kuwa mojawapo ya maswali muhimu zaidi katika darasa la hesabu.

Badala ya mwalimu kuuliza tu, "Jibu ni nini?", anaweza kuongeza: "Umefikiaje hapo?", "Kuna njia nyingine?", au "Kwa nini unafikiri njia yako inafanya kazi?"

Maswali ya aina hiyo yanabadilisha nafasi ya mwanafunzi. Haishii kuwa mtu anayesubiri mwalimu amwoneshe kanuni, bali anakuwa mshiriki katika kutafuta ufumbuzi.

NRICH, mradi wa elimu ya hisabati wa Chuo Kikuu cha Cambridge, unataka wanafunzi wapewe nafasi ya kujitegemea katika fikra na kuthamini mawazo tofauti. Ili kufanikisha hayo, watoo wapewa jukumu la kuchunguza matatizo yasilozoeleka hadi wajenge tabia ya kufikiri kihesabu.

Hii haimaanishi mwalimu aache kufundisha kanuni. Kanuni bado zinahitajika. Kinachobadilika ni kwamba mwanafunzi hatakiwi kuwa mtumiaji wa kanuni bila kuelewa, bali ajenge uwezo wa kuamua ni maarifa gani yanahitajika katika tatizo fulani.

## Si kila swali lina njia moja tu

Katika madarasa mengi, swali huulizwa, wanafunzi wanatafuta jibu moja sahihi, kisha mwalimu anahamia kwenye swali linalofuata. Hiyo ni muhimu katika kujenga umahiri, lakini si lazima iwe njia pekee ya kujifunza.

Wakati mwingine mwalimu anaweza kutoa swali ambalo linaweza kushughulikiwa kwa njia tofauti, au kuwauliza wanafunzi watafute njia nyingine ya kufikia jibu lilelile. Lengo si kuwachanganya. Ni kuwafanya waone kuwa katika hesabu, mara nyingi kuna zaidi ya njia moja ya kufikiri.

Utafiti kuhusu ubunifu katika hesabu unaonesha kwamba maswali yanayofungua nafasi ya njia mbalimbali yanaweza kuwasaidia wanafunzi kujenga uwezo wa kutoa mawazo mengi, kubadili mkakati wanapokwama na kutafuta njia za kipekee za kutatua tatizo.

Kwa mwalimu, mabadiliko hayo yanaweza kuanzia kwenye swali dogo tu: "Nani amefanya kwa njia tofauti?"

## Kukwama ni sehemu ya kujifunza

Mwanafunzi anapokwama, mwalimu anaweza kuwa na kishawishi cha kumwonesha jibu haraka ili darasa liendelee. Lakini wakati mwingine muda anaoutumia mtoto kupambana na tatizo ndiyo sehemu muhimu zaidi ya kujifunza.

NWEA inaeleza kwamba ubunifu katika utatuzi wa matatizo unahitaji muda wa kuchunguza, kujaribu, kushindwa, kubadili njia na hatimaye kupata mwanga wa namna ya kuendelea. Ushirikiano na wanafunzi wengine pia unaweza kuwasaidia kueleza mawazo yao, kusikiliza njia tofauti na kurekebisha fikra zao.

Kwa hiyo, kukwama si lazima kumaanishe mwanafunzi hafahamu. Wakati mwingine ni ishara kwamba anafanya kazi halisi ya kufikiri.

## Mwalimu si mashine ya majibu

Hapa ndipo nafasi ya mwalimu inakuwa muhimu zaidi, si ndogo zaidi.

Mwalimu mwenye ufanisi si yule anayetoa jibu la kila swali kwa haraka. Ni yule anayejua muda gani aeleze, aulize, amsaidie mwanafunzi kwa kidokezo au ampe muda zaidi wa kutafuta mwenyewe.

NRICH inapendekeza pia walimu kuonesha wakati mwingine namna wao wenyewe wanavyofikiri wanapokutana na tatizo. Hii inaweza kuwasaidia wanafunzi kuona kwamba hata mtu mwenye ujuzi anaweza kukwama, kujaribu njia moja, kuikataa na kutafuta nyingine.

Huo ni ujumbe wenye nguvu kwa mtoto anayefikiri kwamba mtu "anayejua hesabu" lazima apate jibu papo hapo.

## Tufundishe fikra, si hatua pekee

Mwisho wa siku, tunataka watoto waweze kujumlisha, kugawanya, kutumia kanuni na kupata majibu sahihi. Lakini tunataka pia waweze kukutana na tatizo jipya na kusema: "Ngoja nifikirie." Huo ndiyo moyo wa hisabati.

Mwanafunzi anayejua kufikiri haogopi sana swali jipya. Anaweza kujaribu njia moja, kuilinganisha na nyingine, kuuliza, kueleza na kurekebisha alikokosea. Hata akichelewa kufika kwenye jibu, anakuwa anajenga uwezo ambao utamsaidia zaidi ya mtihani mmoja.

Kwa hiyo, tunapofundisha hesabu, tusimwulize mtoto tu, "Jibu ni nini?" Mara nyingine tumwulize pia: "Umefikirije?"

Katika makala ijayo tutaondoka darasani kidogo na kuangalia jambo jingine muhimu: Hesabu haikai kwenye daftari pekee—iko sokoni, jikoni, kwenye biashara, michezo, ujenzi na sehemu nyingi za maisha yetu ya kila siku.

Na Junaynat Ally Dama

# Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

## SEHEMU YA 2

## Kupata wazo la habari au kuliendeleza

**Mwandishi anaweza kuwa na wazo zuri lakini bado asiwe na habari. Anaona bei za vyakula zimepanda, Serikali imetangaza mpango mpya, biashara fulani zinafungwa au teknolojia mpya inaanza kutumiwa. Hayo yote yanaweza kuwa mwanzo wa habari, lakini bado yanahitaji kufanyiwa kazi.**

**Swali linalofuata huwa: Habari yenyewe iko wapi? Tunataka kuchunguza nini? Nani anaathirika? Ni swali gani muhimu ambalo halijajibiwa? Hapa ndipo akili bandia (AI) inaweza kuwa na msaada. Si kwa kumwandikia mwandishi habari, bali kwa kumsaidia kulipanua wazo, kulichunguza kutoka pande tofauti na kutafuta mwelekeo bora wa kuripoti.**

### Wazo hadi muelekeo mahsusi

Tuseme mwandishi ana wazo: "Gharama za maisha zimeongezeka." Hilo ni eneo kubwa sana. Mwandishi anaweza kuitumia AI kama sehemu ya kutafakari. Anaweza kuiuliza: Ni maeneo gani muhimu ambayo mwandishi anaweza kuchunguza katika habari kuhusu kupanda kwa gharama za maisha? Ni watu gani wanapaswa kuzungumza? Ni maswali gani yanahitaji majibu?

AI inaweza kutoa mawazo mengi kwa haraka. Baadhi yatakuwa ya kawaida, mengine yanaweza kumfanya mwandishi aone upande ambao hakuwaza. Lakini hapo ndipo kazi ya mwandishi inaanza, si kuishia.

Habari nzuri mara nyingi huwa na mwelekeo mahsusi wa habari (angle). Mwandishi hawezi kueleza kila kitu kuhusu jambo moja katika habari moja. Analazimika kuamua jambo gani muhimu zaidi analotaka kuchunguza na kumweleza msomaji.

AI inaweza kusaidia kutengeneza mwelekeo kadhaa kutoka katika wazo moja. Mwandishi kisha anaweza kuzipima kwa kuangalia umuhimu wake kwa jamii, upatikanaji wa taarifa, watu wa kuhoji na thamani ya habari kwa wasomaji wake.

Hapo uamuzi unabaki kwa mwandishi.

### Inaweza kukusaidia kuona watu waliowasahau

Mwandishi akiwa na haraka anaweza kuwafikiria watu wale wale ambao mara nyingi tunawaona katika habari: kiongozi wa Serikali, mtaalamu na mwakilishi wa taasisi fulani. Lakini habari inaweza kuwa na wahusika wengine muhimu.AI inaweza kutumiwa kuuliza: Ni makundi gani yanaweza kuathiriwa na suala hili lakini yakasahaulika katika habari?

Kwa habari kuhusu kupanda kwa gharama za maisha, kwa mfano, inaweza kukukumbusha kufikiria wafanyabiashara wadogo, wazee, wanafunzi, watu wenye ulemavu au familia zenye watoto wengi.

Haimaanishi kwamba kila kundi litakuwa muhimu katika habari hiyo. Lakini zoezi hilo linaweza kumsaidia mwandishi kujiuliza kama amesikiliza sauti zinazohitajika.

### Tumia AI kutengeneza maswali, si majibu

Hapa kuna matumizi yenye thamani kubwa zaidi. Badala ya kuiuliza AI, "Kwa nini bei zimepanda?" na kisha kuchukua majibu yake kama ukweli, mwandishi anaweza kusema:

"Ninajiandaa kuripoti kuhusu ongezeko la bei za vyakula. Nisaidie kuandaa maswali ambayo ninapaswa kuyajibu kupitia takwimu, nyaraka na mahojiano." Tofauti ni kubwa.

Katika mfano wa kwanza, AI inaombwa kutoa jibu. Katika wa pili, inaombwa kusaidia mwandishi kujenga njia ya kulifikia jibu mwenyewe.

Inaweza kupendekeza kuuliza kuhusu mwenendo wa bei kwa kipindi fulani, gharama za uzalishaji na usafirishaji, upatikanaji wa bidhaa, athari kwa walaji na hatua zinazochukuliwa na mamlaka. Mwandishi ndiye atakayetafuta taarifa hizo katika vyanzo halisi.

### Inaweza kuwa mshirika wa kupima wazo

Wakati mwingine mwandishi tayari ana mwelekeo anaouamini. AI inaweza kutumiwa kuujaribu. Anaweza kuuliza: "Ninataka kuripoti suala hili kwa mtazamo huu. Ni maswali gani ambayo mwelekeo wangu haujajibu? Ni hoja gani zinazoweza kuupinga? Ni watu gani ninaweza kuwa nimewasahau?"

Hii inaweza kumsaidia kuona mapengo kabla hajaanza kuripoti.

Lakini pia kuna tahadhari. AI inaweza kupendekeza mitazamo iliyozoeleka na kukosa uhalisia wa eneo husika. Inaweza kutokuelewa vizuri mazingira ya Tanzania, tofauti za kijamii au jambo ambalo mwandishi anayefanya kazi eneo hilo analijua kutokana na uzoefu wake.

Kwa hiyo, mapendekezo yake yanahitaji kupimwa kwa uamuzi wa kiandishi.

AI isikufanyie kazi ya kuona habari

Kuna hatari nyingine. Mwandishi akizoea kila siku kuanza kwa kuuliza AI, "Nipe mawazo ya habari," anaweza taratibu kupunguza tabia muhimu ya mwandishi ya kuangalia jamii na kugundua jambo mwenyewe.

Mawazo mazuri ya habari yanatoka pia katika kusikiliza watu, kusoma nyaraka, kufuatilia takwimu, kutembelea maeneo, kuzungumza na vyanzo na kujiuliza kwa nini jambo fulani linatokea.

### AI isiwe macho ya mwandishi

Itumike pale inapohitajika kupanua kile ambacho mwandishi tayari anaona, kukichunguza zaidi au kujaribu njia nyingine za kukitazama.

Unaweza kusema: "Nina wazo la habari kuhusu ongezeko la gharama za maisha. Nisaidie kutengeneza mwelekeo mitano tofauti wa habari. Kwa kila mmoja, onesha swali kuu la kuripoti, watu ninaoweza kuwahoji na aina ya taarifa ninayohitaji kuthibitisha. Usitengeneze takwimu wala madai kama ukweli."

Baada ya hapo, usichague tu pendekezo linalosikika vizuri. Jiulize: Ni lipi lina umuhimu kwa jamii yangu? Ninaweza kulithibitisha? Linaongeza nini ambacho wasomaji hawajakijua?

Na Junaynat Ally Dama

# Siku ya Kuzuia Kujiua Duniani: Usijiue, vunja ukimya usaidiwe

WIKI hii dunia imeadhimisha Siku ya Kuzuia Kujiua Duniani, Septemba 10, huku Shirika la Afya Duniani (WHO) likisisitiza ujumbe mmoja muhimu: tubadili namna tunavyozungumza kuhusu kujiua, na tuanze mazungumzo.

Kaulimbiu ya mwaka 2026 ni mwendelezo wa kampeni ya miaka mitatu ya WHO ya "Changing the Narrative on Suicide", yaani kubadili simulizi kuhusu kujiua. Lengo lake ni kupunguza ukimya, unyanyapaa na imani potofu, na badala yake kujenga mazingira ambayo mtu anayepitia msongo mkubwa anaweza kuzungumza na kupata msaada.

Hili si jambo dogo. WHO inasema zaidi ya watu 720,000 hufariki kutokana na kujiua kila mwaka duniani. Kujiua pia ni sababu ya tatu kuu ya vifo kwa vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 29. Takribani asilimia 73 ya vifo hivyo hutokea katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati.

Hivyo kujiua si tatizo la mtu mmoja pekee. Ni suala la afya ya umma. Kifo kimoja huacha maumivu kwa familia, marafiki, sehemu za kazi na jamii nzima. WHO inaeleza kuwa athari zake zinaweza kudumu kwa muda mrefu kwa wale wanaobaki nyuma.

## Si sababu moja pekee

Ni muhimu pia kuvunja dhana kwamba mtu hujiua kwa sababu moja rahisi.

WHO inaeleza kuwa kujiua kunasababishwa na changamano nyimgi tofauti. Inaweza kuwa matatizo ya afya ya akili, matumizi ya pombe, maumivu ya muda mrefu, migogoro ya mahusiano, matatizo ya kifedha, ukatili, kupoteza mtu au kitu muhimu, majanga, migogoro na hali ya kutengwa kijamii.

Katika baadhi ya matukio, mtu anaweza kufanya uamuzi wa haraka wakati wa kipindi kikali cha msongo, pale uwezo wake wa kuona njia nyingine ya kutatua tatizo unapopungua. Ndiyo maana kauli kama, "Alikuwa na kila kitu, kwa nini afanye hivyo?" mara nyingi hazisaidii. Hatuwezi kujua kila mara kiwango cha maumivu anayopitia mtu kwa kumtazama kwa nje.

## Kuzungumza hakuongezi hatari

Moja ya hofu zinazoweza kuzuia watu kuanzisha mazungumzo ni kwamba kumuuliza mtu kuhusu mawazo ya kujiua kunaweza kumpa wazo hilo. WHO inasema mazungumzo ya wazi yanaweza kufanya kinyume chake.

Kuzungumza kuhusu kujiua kunaweza kumpa mtu nafasi ya kuona njia nyingine, kutafakari upya uamuzi wake na kupata msaada. Hivyo unapogundua mtu yuko katika maumivu makubwa, usikimbilie kutoa hukumu au hotuba ndefu.

Wakati mwingine jambo la kwanza analohitaji ni mtu wa kumsikiliza kwa makini na bila kumhukumu.

## Watu wengi hawataki kufa; wanataka maumivu yaishe

WHO inaeleza kuwa watu wanaopitia mawazo ya kujiua mara nyingi huwa na mgongano wa hisia kuhusu kuishi au kufa. Mara nyingi wanatafuta namna ya kuondokana na maumivu makali wanayopitia.

Msaada wa kihisia unaopatikana kwa wakati unaweza kuzuia kifo. Tafiti za watu walionusurika katika majaribio hatari ya kujiua zinaonesha kwamba wengi wao baadaye hufurahi kwamba waliendelea kuishi.

Ujumbe huo una uzito mkubwa: hali ya sasa inaweza kuwa nzito sana, lakini si lazima iwe hali ya kudumu.

## Dalili zisipuuzwe

WHO inataja miongoni mwa hali ambazo zinaweza kuambatana na mawazo ya kujiua: maumivu yanayoonekana kutovumilika, kukosa matumaini, kujiona huna thamani, upweke, mawazo hasi yanayoendelea na kuona kana kwamba hakuna njia nyingine ya kutatua matatizo.

Hizi ni ishara za msongo mkubwa wa kihisia na zinahitaji msaada, si dhihaka. Mtu anaposema maisha hayana maana, anajiona mzigo kwa wengine au anaonesha kukata tamaa kupita kiasi, maneno hayo yanastahili kuchukuliwa kwa uzito.

## Tunaweza kufanya nini?

WHO inapendekeza hatua kadhaa za kuzuia kujiua, zikiwemo kupunguza upatikanaji wa njia hatari zinazoweza kutumiwa kujiua, uandishi wa habari wenye kuwajibika, kuwajengea vijana stadi za kijamii na kihisia, pamoja na kutambua mapema, kutathmini, kutibu na kufuatilia watu wenye tabia au mawazo ya kujiua.

Lakini kinga pia inaanzia karibu nasi. Kama mtu anaonekana kuvunjika moyo, muulize anaendeleaje. Msikilize. Usimfanye ajione dhaifu. Mhimize kuzungumza na mtu anayemwamini au mtaalamu wa afya.

Kwa anayepitia mawazo ya kujiua au kujidhuru, WHO inashauri azungumze na mtu anayemwamini, daktari, mtaalamu wa afya ya akili, mshauri au mfanyakazi wa kijamii. Ikiwa kuna hatari ya haraka ya kujidhuru, anapaswa kupata msaada wa dharura mara moja.

Siku ya Kuzuia Kujiua Duniani inatukumbusha kwamba kuzuia kujiua si kazi ya hospitali pekee. Ni jukumu la familia, shule, sehemu za kazi, viongozi, vyombo vya habari na jamii kwa ujumla. Na wakati mwingine hatua ya kwanza kabisa ni ndogo: Kumuuliza mtu, "Uko sawa kweli?"—halafu ukawa tayari kusikiliza jibu lake.

# Namna ya kuomba msamaha kidhati na kumaanisha

**TUNAPOMUUMIZA mtu, mara nyingi tunafikiri neno moja linaweza kumaliza kila kitu: "Samahani." Lakini mtu anaweza kusema samahani na bado asichukue jukumu. Anaweza kuomba msamaha huku akijitetea. Anaweza kutaka mazungumzo yaishe haraka bila hata kuelewa maumivu aliyosababisha.**

**Ndiyo maana msamaha wa kweli si neno. Ni mchakato.**

**Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa msamaha wa dhati unahitaji mtu akubali alichofanya, atambue athari zake, aoneshe majuto bila visingizio na aeleze atakavyofanya tofauti baadaye. Lengo lake si kufuta kilichotokea, bali kusaidia kurejesha uaminifu na kuonesha dhamira ya mabadiliko.**

**Kwa kuunganisha mitazamo ya wataalamu mbalimbali, msamaha wenye maana unaweza kujengwa kwenye hatua nne rahisi.**

## Mosi, msamaha utaje kosa

Msamaha uanze kwa kutaja kosa. "Nasikitika kwamba nilifanya..." Si sawa kusema: "Samahani kama ulijisikia vibaya," bali sema: "Nasikitika kwa maneno niliyokuambia mbele ya watu."

Tofauti yake ni kubwa. Sentensi ya kwanza inaweza kuonekana kama tatizo ni hisia za mwingine na ya pili, inasema: nilifanya jambo, lilikuwa kosa langu.

Moja ya misingi muhimu zaidi wa msamaha ni kuchukua jukumu bila kuhamisha lawama. "Nilikuwa nimekasirika," "ulinichokoza," au "nilifanya hivyo kwa sababu yako" vinaweza kueleza mazingira, lakini visiwe njia ya kukwepa wajibu.

Utafiti unaorejelewa katika chanzo kingine unatenganisha vipengele vitano vya msamaha mzuri: majuto, maelezo ya kilichotokea, uwajibikaji, ahadi ya kubadilika na kurekebisha madhara. Maelezo yanaweza kutolewa, lakini yasigeuzwe kuwa kisingizio.

## Pili, eleza athari

Baada ya kukiri kosa, jaribu kueleza athari yake. "Naelewa kwamba nilichofanya kilikufanya..." "Naelewa kwamba kutokutambua mchango wako mbele ya wengine kulikufanya ujisikie kama sikuthamini." Hapa unaondoka kwenye swali la "nilimaanisha nini?" na kuingia kwenye swali muhimu zaidi: "kitendo changu kilitengeneza athari gani kwako?"

Misamaha mingi hushindwa kwa sababu mtu hajitahidi kueleza kwa usahihi namna kitendo chake kilivyomuumiza mwingine. Maneno yana maana, lakini thamani yake hutegemea kama yanaambatana na utambuzi wa maumivu yaliyosababishwa na hatua zinazofuata.

Hata kama hukumkusudia kumuumiza mtu, athari inaweza kuwa halisi. Nia nzuri haifuti maumivu.

## Tatu, mpe fursa aseme zaidi

Hii ndiyo sehemu ambayo misamaha mingi hukosa. Baada ya kusema samahani, usijione umefunga mjadala. "Nieleze zaidi..." ni muhimu. Muulize: "Nieleze zaidi kuhusu ulivyojisikia." "Kuna jambo jingine nililokufanyia ambalo sijalielewa?" Kisha nyamaza na usikilize.

Inashauriwa anayeomba msamaha aweke pembeni utetezi, hofu na haja ya kujitetea kwa muda ili aweze kupokea maelezo ya maumivu ya mwingine. Hii inaweza kuwa ngumu. Unaweza kusikia jambo usilokubaliana nalo kabisa. Lakini kusikiliza si sawa na kukubali kila tafsiri. Ni kumpa mwingine nafasi ya kueleza uzoefu wake.

Ndiyo maana msamaha kama, "Sawa basi, nimeshaomba samahani, unataka nini tena?" hauponyi. Unajaribu kufunga jeraha kabla halijasafishwa.

## Nne, toa ahadi

Msamaha haujakamilika mpaka uangalie kesho. Hii hi kusema "Nitafanya... / Sitafanya tena..."

"Sitakudhalilisha tena mbele ya watu." "Nitajadiliana nawe kabla sijafanya uamuzi unaotuhusu wote." "Nikianza kurudia tabia hii, nikumbushe; sitakasirika."

Wataalamu wanasisitiza kuwa ikiwa kuna jambo unaloweza kufanya kurekebisha madhara, lifanye. Kama umeharibu kitu, uliza jinsi ya kukirejesha. Kama umevunja uaminifu, uliza ni hatua gani zinaweza kusaidia kuujenga tena.

Hapo ndipo "samahani" inapopata ushahidi. Ahadi bila mabadiliko inaweza kuwa msamaha wa maneno tu.

## Misamaha ambayo haiponyi

Wataalamu wameainisha baadhi ya misamaha isiyoridhisha. Kuna msamaha wa kujitetea: "Nilifanya hivyo kwa sababu nilidhani nakusaidia." Lakini pia, kuna msamaha wa kutaka kukimbia hisia: "Samahani, basi twende nikununulie kitu."

Pia upo msamaha tunauita wa hasira: "Sawa, SAMAHANI! Sasa umeridhika?" Na kuna kujuta kimya kimya bila kukiri kosa, hali inayomwacha aliyeumizwa ndiye mwenye jukumu la kutangaza kuwa kila kitu kimekwisha.

Yote yana tatizo moja: yanakosa utambuzi wa kina wa madhara na uwajibikaji.

## Kuomba msamaha si kukubali kila lawama

Jambo lingine muhimu ni kwamba kuomba msamaha kwa sehemu yako hakumaanishi unakubali kwamba mgogoro wote ulikuwa kosa lako.

Wataalamu wanaonya kuwa watu wakati mwingine wanaogopa kuomba msamaha kwanza kwa sababu wanaona ni kama kukubali kuwa wao ndio "walioshindwa." Lakini unaweza kuchukua jukumu la kosa lako bila kubeba makosa ya mwingine kwa kueleza vema kosa lako (hatua ya kwanza).

Msamaha wa kweli pia unaweza kusaidia kuweka mipaka mipya: namna mtakavyoongea, mambo yasiyokubalika na tabia zinazopaswa kubadilika ili uaminifu ujengwe tena.